# *Neno Lilifanyika Mwili (Taarifa Ya Ziara Ya India)*

Habari za asubuhi, rafiki. Bila shaka ni majaliwa kuwa hapa maskanini tena, asubuhi ya leo. Bila shaka, tunaposafiri kupitia sehemu mbalimbali za dunia, na kadhalika, wakati mwingine unashangaa kama kamwe utarudi tena, lakini kwa . . . na kuona hatari kubwa na majanga na mambo yaliyo mbele. Lakini kama vile Ndugu Neville alivyosema hivi punde, "Bwana atatutunza." Hiyo ni kusema, tunajifunza kumtumaini Yeye kwa ajili ya . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Na asubuhi ya leo, ni ninii . . .

2 Ninaamini kwamba nina upendo wenye kilindi zaidi kwa Bwana Yesu kuliko nilivyowahi kuwa nao katika maisha yangu yote. Baada ya kuona dini mbalimbali za ulimwengu, na shughuli zao na kile wanachoamini, na theolojia yao na kadhalika, na kisha kuja kutambua ya kwamba sisi, kama Wakristo, tunaye Mungu wa kweli na aliye hai. Dini zingine zote zinaonekana kutoweka kabisa, wakati—wakati Ukristo unapoletwa ma—mahali hapo.

3 Sasa, sina sauti kubwa sana, kuongea. Ikiwa mtu yeyote anataka kuja karibu zaidi, mbona, u—unakaribishwa hata na zaidi kuja mbele, wakati tukingojea.

4 Ninataka tu kutoa taarifa ya mkutano wa nchi za ng'ambo, kwa ufupi tu, na ili kwamba muwe na wa—wazo la kile Bwana alifanya huko ng'ambo. Kwa maana sisi ni . . . ninyi ni sehemu ya kundi lililonituma, nanyi mliniombea nilipokuwa huko, kwa hivyo mna haki ya kujua kile ambacho Bwana alifanya. Ilikuwa ni mi—mikutano mikubwa na ya ajabu tuliyokuwa nayo. Wao . . .

5 Katika Ureno; Lisbon, Ureno, tulikuwa na mojawapo ya mikutano bora sana ambayo nilikuwa nayo kwa muda mrefu, kuingia tu kama tulivyofanya. Kwa kweli, ni nchi ya Kikatoliki asilimia mia moja, ndivyo ilivyo Ureno, iliyotoka Uhispania. Nao Wahispaniola walikuwa Wakatoliki, ndipo wakaingia mle. Na Wareno wo—wote ni Wakatoliki. Lakini katikati ya hayo yote, Bwana alimimina Roho Wake juu ya makusanyiko, nasi tulikuwa na mikutano na miujiza ya ajabu sana!

6 Na maelfu mengi, mengi sana . . . Sasa, endapo kuna Wakatoliki hapa, sijaribu kusema kwamba watu waliongoka wakawa Wakristo kutoka katika Ukatoliki; kwa sababu,

ni kiwakilishi cha Ukristo. Lakini, wao, watu ambao kwa kawaida huhudhuria ka—kanisa Katoliki, wala si Wakristo waaminifu kweli; tunao katika Waprotestanti, pia; wanasema tu, "Vema, mimi ni Mkatoliki kwa sababu nyanya yangu alikuwa Mkatoliki." Na, ndivyo hivyo, ha—hawauzingatii. Lakini watu hawa, namna hiyo, waliongozwa kwa Bwana Yesu Kristo, kwa maelfu, katika huo mkutano wa huko Ureno.

7 Kisha tukatoka huko kwenda Rumi. Na mara. . . Vema, nikayatembelea makaburi makubwa ya mapangoni ambamo Wakristo waliabudia, hapo mwanzoni, nyakati za mwanzoni. Na huko tulikuwa na tukio la ajabu sana, kushuka chini, hasa katika Makaburi ya mapangoni ya Mtakatifu Angelo. Na, bila shaka, viongozi wetu walikuwa Wakatoliki wa dhati. Lakini walijaribu kusema hao walikuwa Wakatoliki, lakini maandishi yote na kila kitu kilionyesha kuwa ilikuwa vinginevyo; sivyo, mnaona.

8 Halafu kutoka humo tukaenda kwenye Jiji la Vatikani. Na katika Jiji la Vatikani, nilikuwa na wakati mzuri sana. Pia tukawa na ibada ya uponyaji, papo hapo kwenye vivuli vya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro kule; mkutano mkubwa. Na kwa kweli wote tu ambao wangeweza kuwapata huko, ambako tulilazimika kuufanya kwa siri, na kuwajulisha tu watu mahali tulipo. Ndipo maelfu wakajitokeza na kumkubali Bwana Yesu Kristo, Naye akafanya miujiza na ishara na maajabu miongoni mwa watu. Katika . . . kwenye Jiji la Vatikani, mwaweza kuwazia hilo?

9 Nami ningeweza. . . ambapo nilikutana na watu wengi mashuhuri wa nchi wakati huu, kwa sababu Baron von Blomberg alikuwa pamoja nasi, alikuwa ndiye meneja wa mkutano, naye anajulikana sana na wafalme wote, na watawala, na kadhalika, wa ulimwenguni. Huko Lisbon, mbona, tulikutana na gavana wa bunge, tukala chakula cha jioni pamoja nao. Na huko Rumi, waheshimiwa wote huko.

10 Na huyu Mfalme Farouk, Farouk, lolote lililokuwa jina lake, wa kutoka Misri, ambaye ndiyo kwanza amwoe msichana mdogo, mwajua, tulisikia, kisha wakatalikiana tena. Na ana haki ya kuwa na wake wanne, kwa hiyo a—ana kama mke mmoja au wawili tu sasa. Lakini, alimwoa msichana huyu mdogo, msichana wa shule, nanyi mkayasikia hayo matangazo kwenye gazeti, na kadhalika. Mtu mzuri wa kuzungumza naye. Jamaa mkubwa, mkuu . . . namaanisha, jamaa mkubwa! Alikuwa mkubwa. Kwa hiyo a—alikuwa mtu mzuri.

11 Kisha tukakutana na malkia kadhaa wa huko Mashariki, na kadhalika. Halafu basi walikuwa huko Rumi, nao wakijua ya kwamba tulikuwa kule, wakaja kukutana nasi.

12 Nami nilikuwa na mkutano na papa, na ningaliweza kwenda na kuzungumza naye. Lakini nilipogundua ilibidi ubusu pete yake na kidole chake cha mguu, nilisema, "La, la. Huh-uh! La."

Mnaona? Nitampa mtu yeyote heshima zake, kama mchungaji, daktari, chochote alicho, kumpa heshima, na kumvulia kofia yangu, kama mwungwana, ama kadhalika. Lakini inapofikia kuabudu, kuna Mmoja tu, huyo ni Bwana Yesu Kristo. Nami nisingeweza kufanya hivyo.

13 Kwa hiyo akasema alikuwa amemwuliza, akamwuliza yule baroni, na kadhalika, kama angenipeleka kule Jumanne alasiri, ama kitu kama hicho. Akasema, "Sasa unapoingia," kasema, "jambo la kwanza unalofanya, unainama mbele zake. Kisha anainua pete yake, nawe unaibusu pete yake. Kisha anaunyosha mguu wake, na kidole kwenye huo."

14 Nikasema, "La, la, la. La, bwana. Sahau tu hilo. Hatutafanya hivyo."

15 Kwa hiyo basi tukaendelea mpaka Cairo, Misri, na Athens, Ugiriki, tukashuka kuingia—kwenda sehemu mbalimbali za nchi, ndipo tukamalizia Bombay. Nami nawaambia, siamini ya kwamba ningeweza kusahau yale niliyoyaona huko Bombay, katika miaka kumi, jinsi yalivyokuwa. Mimi . . . Ndiyo tamasha ya kusikitisha kuliko zote ambayo nimewahi kuona maishani mwangu, kutoka kote ulimwenguni.

16 Hii kwa kweli ndiyo upeo wa Mashariki ya mbali. Nilitembelea nchi zote za Uropa na Asia, na—na kupitia sehemu hiyo ya nchi, hata kwenye mipaka ya Urusi, lakini sijawahi kwenda Japani bado. Na hiyo inapaswa kuwa inayofuata kwenye ratiba, hii, Australia na Nyuzilandi na Japani. Kituo changu cha pili, kutoka mahali nilipokuwa, kilikuwa Hong Kong, Uchina. Tulikuwa tumezunguka tu upande ule mwingine, karibu sana na Marekani, tukija *hivi*. Ilitubidi tu kusimama Hong Kong, Tokyo, Formosa, na Guamu, Wake, Ufilipino, kisha hapa. Badala ya hilo, tunarudi moja kwa moja kuzunguka kupitia njia hii nyingine, kuingia—kuingia tena. Lakini huko ndani . . .

17 Hakuna watu masikini Marekani. Sijali yuko wapi, na jinsi anavyolazimika kuishi maisha magumu, hakuna kamwe, hakuna hata maskini mmoja Marekani. Ukimkuta kwenye uchochoro, akila kutoka kwenye pipa la taka, amevua nguo zake zote, na chochote kile, yeye ni milionea. Kamwe usifikirie kuwa yeye ni maskini, maana sivyo alivyo; ukiisha kuitembelea India mara moja, utawaona maskini huko. Mbona, nakwambia, ninii ngumu . . .

18 Nina moyo mgumu. Nimeona mengi na ilibidi kupitia mengi. Huenda wengi wenu msielewe ni jinsi gani, athari iliyo nayo kwa mwanadamu, unapoona mambo mengi sana, nawe huna budi kutembea juu yake, wakati wote, namna hiyo, ujifanye kusikia tofauti. Baada ya muda, unaingia kwenye mazingira ya aina hiyo, mpaka unayaangalia mambo wala huyaoni, maana u—u—umejifikisha mahali hapo.

19 Kama vile daktari, inamlazimu kumfanyia mtu upasuaji, anaingiza mkono na kutoa kidole tumbo chake. Mara ya kwanza alipofanya hivyo, labda alizimia au chochote kile. Lakini baada ya kitambo kidogo, anafika mahali, anajua hauna budi kufanywa, kwa hiyo anaenda tu na kuufanya. Basi kama mgonjwa akiishi au akifa, mbona, yeye ananinii tu, amefanya vizuri awezavyo.

20 Na ni vivyo hivyo kwa mhudumu, wakati wewe. . .hasa sana mtume. Au—au, kile. . .Vema, mtume ni mmishenari. Neno misheni-. . .*mtume* maana yake ni "mtu aliyetumwa." Na kwamba ni kwa nini mmishenari anataka kuitwa mmishenari, badala ya mtume, sijui mimi. Agizo lake la Biblia, ni, ni mtume. Na hivyo basi anatumwa nje. Sio lazima kabisa awe mhudumu. Yeye. . .mtume si lazima awe mhudumu; inabidi tu awe mtu aliyetumwa. Mungu alimtuma kufanya mambo fulani.

21 Na halafu huko ndani, nawaambia, tulipoingia India, na kuwaona hao watu maskini wamelala barabarani, na wakifa kwa njaa. Na maskini akina mama na watoto wao wachanga, huku wakiomba kitu. Nao wanakufa, wao wenyewe, kwa ukosefu wa chakula, bali hawamwachi mtoto wao mchanga afe. Na kwa kidogo tu, senti ishirini na tano, mashilingi, ama chochote kile. Endapo wanaweza kupata chakula kiasi hicho kila baada ya siku tatu, wanaweza kufaulu. Hawana nyumba ya kwendea. Wakishikwa tu na usingizi, wanalala mtaani. Nao. . .maskini mgongo mkali, labda, hawaufikii ukubwa *huo*, na mbavu zake zimekunjamana kwa ukosefu wa chakula, wakitembea-tembea juu ya watu. Na mbuzi mkongwe, naye anapepesuka vibaya sana, pia, akitembea-tembea juu ya watu. Nao wanavunda. Na, loo, hujawahi kuona vurugu kama India ilivyo! Kwa kweli, sikuzote imekuwa hivyo. Si chochote kipya.

22 Ndio kwanza wapate uhuru wao yapata miaka sita iliyopita, wakiwa wamefilisiwa na Uingereza, kama mnavyojua. Nao ni—ni watu wa kipekee sana.

23 Sijawahi kuona mtu mmoja India nzima, kwa mamilioni wote niliopata kuona, aliyekuwa na viungo, popote juu ya paja lao, juu hapa, vikubwa *hivyo*; wote ni watu waliokonda sana, magofu ya watu. Na kwenye dirisha langu, ingevunja moyo wa mtu, mwanangu akiwa ameketi kule nyuma, akisikiliza. Naye aliketi dirishani na kuangalia watu wameketi mitaani. Walipogundua mahali nilipokuwa, na wenye ukoma wasio na mikono, vitu kama vigutu vidogo vimeinuliwa hewani, wakiomba chakula, ama chochote kile; wala hawana miguu, na ni weupe kwa ukoma. Na, loo, ni, mmoja asingeweza kumsaidia mwingine, ni vigumu. Na, loo, ni mandhari ya kusikitisha sana uliyowahi kuona!

24 Nami nikawaambia wamishenari, nikasema, "Siwezi kabisa kulivumilia." Nikasambaza kila senti niliyokuwa nayo, kwao, na

kila kitu, mitaani. Nami ni—ni—nikawazia, "Wana haki ya kula kadiri Sarah wangu na Rebekah walivyo nayo."

25 Na—na—nanyi kamwe hamtambui jinsi mlivyobarikiwa, enyi watu. Sasa, hiyo ni kweli, hamtambui. Mnajua, mnapaswa kuangalia juu na kuona zinakotoka. Jamani! Zinakuja . . . Nao Wamarekani ni kama nguruwe chini ya mtofaa. Mnajua, yeye . . . mchana kutwa matofaa yatamgonga kichwani, naye atayala, na kamwe hataangalia juu kuona yanakotoka. Na hivyo ndivyo tulivyo. Kamwe hatuliwazii, namaanisha, kwa ujumla; simaanishi ninyi watu hapa. Ninyi ni Wakristo. Lakini na—namaanisha watu kwa jumla, jinsi wanavyoninii tu . . . hawa—hawatambui jinsi walivyobarikiwa na jinsi walivyo na hali bora zaidi.

26 Takataka za Jeffersonville zingelisha, leo hii, zingelisha robo ya India. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, nao wangefurahi kuzipata, chochote. Wao . . .

27 Unamwona mtu kwenye pipa la takataka; unasema, "Vema, Ndugu Branham, vipi kuhusu jamaa *yule*? Karibu yu uchi, na mchakavu." Lakini, angalia, jambo pekee analopaswa kufanya ni kuomba wahisani, nao wangemsaidia. Yule jamaa hana hisani, kule. Yeye, hasa, anaishi katika kibanda mahali fulani, ambapo, mvua ikinyesha, anaweza kuingia kwenye behewa.

28 Hana pa kwenda. Aangukapo, analala tu hapo. Nao huwaokota wanapokufa, na kuunguza hizo maiti, wanazitupa kwenye shimo kubwa, ama mahali fulani kama hapo, na kuwaondosha mitaani, ama chochote kile; wenye ukoma, na kadhalika. Hakuna anayewataka. Hakuna mahali pa kwenda. Hakuna kitu. Wana njaa. Wao ni wanadamu sawa tu na sisi.

29 Nami nakwambia, ndugu, ni—nisingeweza kulivumilia. Karibu niingie wazimu. Nami nimekuwa nyumbani sasa, siku hizi zote, tangu Jumapili iliyopita. Wala nisingeweza kutoka chumbani. Mke wangu pale anajua ukweli, kwa takriban siku tano. Karibu liniue. Hata daktari wetu aliponipima shinikizo la damu, alisema, "Jamani, afadhali ukapumzike kidogo." Kasema, "Mishipa yako iko chini sana hata shinikizo lako la damu limeshuka sana, wala hata halitaichukua, halitaipandisha damu yako, namna hiyo, ili irudi juu tena." Mimi . . . Nusura inivunje vipande viwili, kuona mambo kama hayo.

30 Ndipo, hilo, basi baadhi ya wamishenari wakasema, "Ndugu Branham, iwapo jambo hili linakuumiza hivi, usiende bara kamwe, maana ni kubaya zaidi mara nyingi, nyingi sana kuliko huku." Bombay ndilo jiji lao kubwa kuliko yote, na jiji zuri sana walilo nalo. Nawe unapaswa kuliona!

31 Na sasa kuhusu dini zilizo upande huo, sijapata kuona kama huo, ushirikina mwingi sana! Watu, vipofu kabisa, kutokana na kutazama jua, kuabudu jua; wanaingia tu upofu, wakilitazama jua.

32 Nilikaribishwa kule na, vema, waheshimiwa, hiyo ni kweli, kuanzia kwa Bw. Nehru, na rais, na bunge na hao wote. Nina tiketi zao na kadhalika, papa hapa mfukoni mwangu, kadi zao ndogo, na kadhalika. Walikuwa wazuri. Wasingeweza kuwa wazuri zaidi. Kukutendea mema.

33 Lakini nilienda kwa meya wa Bombay, ofisini mwake. Banda lako la kuku linaonekana bora zaidi, unaona, kutokana na mazuri kuliko yote waliyokuwa nayo. Na kwa hivyo hakuna chakula. Na mitaani, ni jambo la kusikitisha sana ulilowahi kuona. Mnapotuma vifurushi vyenu vya "msaada," vitumeni India. Naam, bwana.

34 Sasa, siko hapa kama mkosoaji. Nilimwambia mke wangu, nikishuka huku, "Kwa vyovyote vile, nataka kuacha," na kuliomba kanisa hili liniombee, "ni kuachana na ukosoaji." Mimi ni mkosoaji moyoni mwangu, nami si—simaanishi kuwa hivyo.

35 Mara tu nilipougusa udongo wa Marekani, kabla sijafika hapa, niliwaona Wamarekani na kuanza ukosoaji mara moja, nilipotazama na kumwona maskini mama mkongwe akiwa nyuma ya ndege. Tulikuwa tunasafitri daraja la pili, jinsi, kwa kweli, wahubiri wanavyopaswa kusafiri. Na nyuma ndani ya ndege, maskini mama mmoja huko nyuma na watoto wadogo, na huyu jamaa alikuwa ameketi pale akiwagombeza hao watoto kwa sababu wao. . . tulikuwa. . . Nilikuwa hewani kwa saa hamsini na nane. Lakini wao. . . nao walikuwa wameingia karibu—karibu saa thelathini na tano; maskini jamaa hao wadogo, wakihangaika, na hao wakipiga makelele.

36 Na kisha kuwaona wanawake Wamarekani wakisimama, wamevalia kizinifu sana! Hata kwa utu wao mzinifu, kukosa kwao—kwao chakula, hao wanawake wanaweza kuja hapa na kuwafundisha wanawake hawa Wamarekani jinsi ya kuishi kwa adabu. Hiyo ni kweli. Wewe kamwe. . . Mtaani, sijali kama ni mkeo, huwezi kusimama ndani ya inchi sita kutoka kwake. Watakutia ndani, unaona, hiyo ni kweli. Hakuna kuchumbiana na kufanya mapenzi, na kadhalika, mitaani humo. Wala wanawake wao kamwe hawamtazami mwanamume usoni mwake, wanapozungumza naye, wanainamisha vichwa vyao *hivi* na kuondoka. Wala wao—wala hawawaachilii mtaani namna hiyo, na kadhalika. Na ni maadili. Ndipo kuja kukutana na watu wanaokufa kwa njaa, na ni makafiri, tuseme, jinsi hao walivyokuwa, na kuona sehemu duni, iliyojivunjia heshima ya taifa letu hapa, inanifanya mkosoaji.

37 Na mimi—mimi nilisimama hotelini, Taj, Taj Mahal. Nadhani Billy. . . Je, unatamkaje hilo, Billy? Ungeninii vipi. . . Billy Paul, unatamkaje hilo, Hoteli ya Taj Mahal? [Ndugu Billy Paul anasema, "Taj Mahal."—Mh.] Taj Mahal, naam, kwa vyovyote vile, na ho—hotelini kule. Naye Billy ni shahidi.

38 Wamarekani wawili waliingia. Nao walipoenda mtaani . . . Tuliwaangalia walipokuwa wakitoka, nao wakatembea kati ya hao watu maskini huko nje. Ndipo maskini mvulana mdogo akawakimbilia. Kuna namna fulani ya ugonjwa wanaopata. Alikuwa na umri wa miaka minane hivi. Kidole chake cha mguu kilikuwa kikubwa *hivyo*, viwili kati yake; vilitokeza juu *hivi*, naye ilimbidi kukokota miguu yake midogo namna *hiyo*. Akapanda kule na kuomba senti, mwajua, ama kitu kama hicho, akajinunulie chakula. Nao wale Wamarekani wakasema . . . [Ndugu Branham anaashiria na kuiga kuitika kwao.] Waligeuka namna hiyo, wakaenda zao.

Nikasema, "Mungu, uturehemu."

39 Wakaidi! Naye Nehru na hao wengine walikuwa wakizungumza nasi, kasema, "Tungependa kuwa na njia zenu zote ya jinsi ya . . . na demokrasia yenu, na kadhalika namna hiyo, lakini hatutaki roho yenu." Hiyo ni kweli. "Hatutaki majivuno na kujigamba mliko nako huko Marekani. Hatutaki." Mnaona? Wala hawakusita kutwambia. Kasema, "Hatutaki hayo."

40 Nami nikasema, "Huo si uwakilishi wa kweli wa Ukristo." Nikasema, "Huo ni mfano wa unafiki." Kweli kabisa. Nikasema, "Wakristo hawatendi hivyo. La, bwana." Nikasema, "Sio wote Marekani wanaofanya hivyo." Nikasema, "Tuna watu wanyenyekevu na watamu tu kama walivyo popote ulimwenguni. Lakini tuna wengine . . . " Nikasema, "Na—nasikitika, kusema hivyo," Nikasema, "wengi wao, na walio wengi sana, ni wenye kujigamba, wakaidi, wenye kujivuna, namna hiyo."

41 Basi kuja hapa, kunanifanya mkosoaji, mnaona, wala sitaki kuwa hivyo. Nami nikagundua, baada ya mengi sana, kuona mengi sana, na kila kitu namna hiyo, mpaka, ndugu na dada, marafiki zangu wa zamani hapa kutoka maskanini, nawatakieni heri. Hamtambui nilichopitia. Siku zangu za kujaribu kuwalisha na kila kitu. Na nikijaribu kufanya vizuri sana niwezavyo kuwajibika mbele za Mungu siku moja. Lakini nina . . . Kwa hivyo mkiniona nikifanya makosa, msinihukumu, nihurumieni tu, pia mjaribu kunisahihisha, mnaona, maana si—simaanishi kuwa hivyo.

42 Lakini inakulazimu kupitia mengi sana, hutambui, na inakulazimu kuvumilia mengi sana. Ningeweza kuwaambia mambo asubuhi ya leo, ambayo isingekuwa halali kwangu kuwaambia asubuhi ya leo, mngetambua ni kwa nini nilikuwa huko juu siku tano, nyumbani, wala nisingeweza kutembea-tembea. Hiyo ni kweli. Hamtambui.

43 Jinsi, yale yaliyotukia tangu maskini mhubiri asiye na hatia anayesimama hapa mimbarani, kile ambacho kimepitia juu ya moyo huo, na kukata, na kupiga kabisa, na kuvuta. Mungu ndiye

tu ajuaye. Hata siwaambii watu, si hata mke wangu mwenyewe, ninaliweka tu kati yangu mimi na Mungu, na kusonga mbele kadiri niwezavyo. Lakini mnatambua ya kwamba, mwanadamu, akili yake inaweza tu kustahimili kiasi fulani, kisha amekwisha, mnaona. Na kile ambacho kimenishikilia, sijui, imekuwa tu ni Mungu pekee ambaye amefanya hivyo.

44 Sasa, kuna dini za kila namna nchini India. Kila kitu kina dini. Kila kitu kina njia yake. Nilikaribishwa na ninii cha kihistoria. . . Kamwe dini za India, hapo awali, hazijapata kukutana pamoja kumkaribisha Mkristo. Lakini majuma mawili yaliyopita, Alhamisi iliyopita, nilikaribishwa na dini za India.

45 Na wengi wao wanaabudu nzi. Na wanaabudu ng'ombe. Nao wanaabudu, loo, kila kitu. Nao walikuwa pale, Wajaini, tulipokuwa tumeketi pamoja, katika hekalu lao. Ambamo makuhani wao. . . Dini hiyo iliyoanzishwa kabla Ukristo haujazaliwa; miaka elfu tatu au nne iliyopita.

46 Wana nyumba ya watawa, wana watawa, mfano hasa wa Ukatoliki. Wanang'oa ndevu zao kwa mikono yao, na nywele zao vichwani mwao, namna *hiyo*, kwa mikono yao, kisha zinaanza kumea. Huwezi kuzikata.

47 Na wako hivyo kwa kila njia, mpaka wao—wanachukua u—ufagio na. . . au kitu kidogo cha kupangusia. Wanaketi pale; watawa wanatengeneza vitu hivi vidogo vya kupangusia. Nao wanatangulia, namna *hiyo*, kuhakikisha kwamba humkanyagi chungu au kitu fulani, kumwua. Ingekuwa, ingekuwa ni dhambi ya mauti, wala usingesamehewa. Wanabeba kitu cheupe kinywani mwao, na karibu na masikio yao, ambapo, kama wangepumua, itokee wammeze kiroboto mdogo, wasingesamehewa hilo kamwe. Mnaona, i—iliua kitu fulani. Na, loo, jamani!

48 Wangewezaje kukubali dhabihu ya Damu ya Bwana Yesu Kristo? Wamesikia habari Zake, lakini hawaamini. Wanajua habari za Yesu. Wamishenari wanaipeleka. Akasema, "Loo, naam, lakini ninyi watu mmechanganyikiwa kabisa." Kasema, "M—m—mnawazia habari za yule Mtu Yesu. . . Ikiwa alikuwa Mtu mtakatifu, awaache watu waovu wamsulubishe? Upuuzi!" Kasema, "Alipanda farasi akaenda zake Mbinguni. Huko ndiko alikokwenda."

49 Na—nao Makalasinga, wanavaa kilemba; *hapa* ndani wana kisu. Na kila wanapomwona Mkristo ameangalia kwingine, wanamwua. Mnaona, kwa sababu atakapofika Mbinguni. . . Mkristo anaenda mbinguni, pia. Lakini atakapofika Mbinguni, atakuwa Mkristo; atakuwa mtumishi wa Jaini, mnaona. Kwa hiyo angekuwa na watumishi wengi sana kama angeweza kuwaondoa wengi hapa duniani, mnaona. Na kwa hivyo akikuua, umeuawa tu, hakuna lingine. Na nyuma kwenye kilemba chao, unaweza kujua, wana kichanuo kidogo

kinachotokeza hapa, na kisu kimetokeza ubavuni hapo. Nao wanakutaka tu uwape kisogo, hivyo tu ndivyo wanavyotaka kufanya. Halafu, kila kitu tu, dini za ulimwengu!

50 Basi nikiwazungumzia usiku huo, usiku wa kwanza wa mkutano, wakati hapakuwa na njia yoyote ya kukadiria watu waliokuwa pale. Hakukuwa na mahali ambapo ungeweza kuwaweka. Katika monsuni, ambayo ilikuwa ni msimu wa mvua, ilikuwa inaendelea; nao watu wamelala huko nje, na hawajiwezi. Na, loo, magonjwa ya kusikitisha sana. Ndipo ikawa kwamba wa kwanza kuja, na chochote walichoweza kumpandisha juu, alikuwa mvulana mdogo, ambaye alikuwa ninii . . . Ninaamini alikuwa Baniani. Sivyo, Paul? Wala asingeweza . . . mtoto mdogo kiziwi na bubu, naye alizaliwa kiziwi na bubu.

51 Nami nikasema, "Sasa huyu hapa mgonjwa wa kwanza, kijana mdogo hapa." Nikasema, "Sasa kila mmoja wenu, mmoja, hao Wajaini, atajaribu kuwafanya wawe Waislamu; na hao wengine, wanajaribu kukupa vitu tofautitofauti, na . . . ? . . . "

52 Na wote wanasoma Biblia zao walizo nazo, si Biblia hii, nao wanayo Biblia ya Kurani, mnajua hilo. Kwa hiyo wanayo . . . Hiyo ni kupitia kwa Waislamu. Nao wao—wao wana waanzilishi mbalimbali.

53 Sasa, kuna baadhi yao huko wanaoamini, kwamba, "Mtu ni mungu, mwenyewe; kwamba kila mtu ni mungu. Na kadiri ulivyo bora ndivyo ulivyo mungu bora zaidi." Na, loo, i—inatisha kuona jinsi wanavyofanya.

54 Na pale, nikasema, "Sasa angalieni, enyi waungwana," nisingeweza kuwaita ndugu. Niliwazungumzia kama waungwana wa dini za ulimwengu. Mnaona? Nami nikasema, "Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Hapo . . . Sote tuko hapa leo, ama usiku wa leo, hasa. Na mambo haya yote mbalimbali; nanyi mnaabudu ng'ombe, na mnaabudu kila kitu." Nami nikasema, "Yote ni, kunradhi, ushirikina." Wote waliweza kuelewa Kiingereza; wasingeweza kujibu. Lakini, Uingereza imewatawala kwa muda mrefu sana.

55 Nikasema, "Mko—mko hapa, nasi tunaninii . . . Kila mmoja, mnawakilisha dini mbalimbali." Nikasema, "Nanyi mnaenda na kutafuta waongofu. Mnamchukua Ka—Ka—Kalasinga, mkamfanye Mjaini; na mnamchukua Mwislamu, kumfanya M—Mbudha, na kadhalika namna hiyo." Nikasema, "Ni mabadiliko ya fikra tu. Hivyo tu."

56 Nikasema, "Tuna kitu kama hicho Marekani. Hatuna kinga ya mambo haya," nikasema, "lakini sote tunamwamini Mungu mmoja." Nikasema, "Basi, tuna Methodisti, na Baptisti, na Presbiteri, nao wanafanyana waongofu, mmoja kwa mwingine, kuingia katika madhehebu.

57 "Lakini ninyi nyote mnabadilisha mungu mmoja kwa mwingine, mnaona. Lakini," nikasema, "sasa ni ipi? Ni, kila moja, ushirikina."

58 Nikasema, "Kiumbe chenyewe, nzi mnayemwabudu, ng'ombe mnayemwabudu, farasi, au chochote kile, Mungu Mwenyezi aliumba kiumbe hicho, mnaona." Kisha nikasema, "Mnaabudu kiumbe badala ya Muumba, mnaona, kiumbe," nikasema, "katika yote. Sasa, hakuna hata mmoja wao. . . " Huku baadhi yao wana sanamu na kadhalika. Nikasema, "Hakuna hata mmoja wao anayeweza kuwasaidia. Hakuna hata mmoja wao anayeweza kujibu. Wote ni bubu, wala hakuna hata mmoja wao anayeweza kujibu. Hakuna hata mmoja wao anayeweza kufanya vitendo.

59 "Lakini kuna Mungu Mmoja tu wa kweli na aliye hai, na Yesu Kristo ndiye Mwanawe." Kisha nikasema, "Sasa huyo Ndiye niko hapa kumwakilisha."

60 Nikasema, "Sasa, kama vile Eliya, nabii, alivyowaleta manabii wote wa Baali, na kadhalika, kwenye Mlima Karmeli, kuthibitisha na kusema Mungu ni nani," nikasema, "sasa kuna jambo moja tu la kufanya. Na, basi, ikiwa miungu wenu ni sahihi, basi acheni nimwache wangu na kuwatumikia wenu.

61 "Sasa huyu hapa mvulana kiziwi na bubu amesimama. Ni yupi kati ya miungu wenu anayeweza kumponya, ampe—ampe ninii—amfungue masikio na apate kuzungumza? Hilo ndilo ninalotaka kujua. Mnaona? Ni yupi anayeweza kurejesha usemi kwa mvulana huyu?" Na kila mtu alikuwa kimya.

62 Nikasema, "Sasa Ukristo umewakilishwa kwenu, kwa mfano wa mafundisho, na katika vijitabu, na katika Biblia." Ambayo, naiunga mkono, asilimia mia moja. Mungu awasaidie wale wamishenari wanaoenda huko kuishi huko! Naam, bwana. "Lakini," nikasema, "haujawakilishwa kikamilifu kwenu." Mnaona? Nikasema, "Umewakilishwa kwenu, katika Neno pekee. Lakini Mungu aliyeandika Neno hilo, ambalo tayari umeliweka moyoni mwako, sasa amefikia mahali ambapo Yeye atalifanya Neno kuwa hai, mnaona, ajiumbe Mwenyewe katika Neno."

63 Sasa, nikasema, "Huyu hapa kijana amesimama. Yeye ni kiziwi na bubu. Hawezi kuzungumza wala kusikia, au chochote kile. Amezaliwa hivyo." Naye Roho Mtakatifu akiwa pale na kufunua dhambi na kadhalika, hao watu. Nao nusura tu wazimie wakati wangeona hilo, mwajua.

64 Na wote wanapiga kelele nyingi sana, usingeweza kuelewa, maana walikuwa tu na wanamgambo wa kuwaangalia, mwajua. Nao walikuwa tu huku na huko. Loo, jamani! Walisema watu kutoka kote India walikuwepo. Kwa hiyo u—usingeweza kujua waliokuweko, unaona, ni wangapi ama chochote kile, usingeweza kuelewa.

Kwa hiyo basi, basi, mvulana huyu mdogo, nilipomleta pale juu.

65 Basi nikasema, "Sasa, Baba wa Mbinguni, unajua ya kwamba mimi ni kama tu watu hawa wengine hapa. Ningekuwa katika hali yao, na mbaya zaidi, kama haikuwa ni kwa neema Yako, unaona. Uliniokoa. Na mimi—mimi . . . Haya yote yameamriwa na Wewe, si kwa ajili yangu. Na, sasa, unajua ya kwamba kamwe sisemi ya kwamba ninaweza kufanya jambo moja. Ni Wewe, Bwana. Lakini papa hapa, wakati dini na ushirikina wa ulimwengu huu . . . Kama ilivyokuwa katika siku za nabii Eliya, kama ilivyokuwa katika siku za Yesu, Mwanao, ndivyo ilivyo sasa tena."

66 Nikasema, "Kusudi ijulikane, Bwana Mungu, mara nyingine tena, ya kwamba Wewe ndiye Mungu wa kweli na aliye hai, na Yule aliyewaumba wanadamu, na anaweza kuwafanya mabubu kuongea, au viziwi kusikia." Nikasema, "Ninakuomba Wewe, katika Jina la Mwanao, kulingana na Neno Lake; alisema, tukuombe lolote, kama mwaminio Mkristo, 'omba lolote' katika Jina Lake, kwa Baba, utapewa." Nikasema, "Sasa ninaamini Neno Lake, nami ninaomba huyu roho bubu na kiziwi amwache huyu mtoto," namna hiyo.

67 Nami nikapiga makofi namna *hiyo*. [Ndugu Branham alipiga makofi—Mh.] Naye akageuka na kutazama pande zote. Alikuwa ameinua masikio yake juu namna *hiyo*. Naye huyo hapo, angeweza kuzungumza ama kusikia vizuri kama mtu yeyote kwenye hilo kusanyiko, namna hiyo.

68 Naam, hilo likalianzisha! Wa pili, basi usingeweza . . . Ilibidi wanitoe nje. Hakuna njia. Nao wananinii tu . . . Karibu wanivue viatu, wavue nguo zangu. Majeshi hayangeweza kuwazuia. Wanamgambo, walinzi, wasingeweza kuwazuia. Wangekimbia, kweli, wavunje safu hiyo ya walinzi, namna hiyo. Wangekuabudu, unaona, kama—kama wangeweza. Hawaelewi. Haijalishi unajaribu vipi kuwaelezea, hawaelewi.

69 Aliyefuata alikuwa ni mwanamume, kesho yake jioni, alikuwa ni mtu aliyekuwa kipofu, loo, takriban miaka ishirini ama thelathini, mwabudu jua, akilitazama jua mpaka macho yake yakapofuka. Ilikuwa *hivyo*, akilitazama jua moja kwa moja, mpaka akapofuka kabisa. Hakuwa ameona miaka ishirini au thelathini. Ilitokea kwamba yeye ndiye aliyefuata, akazunguka akaja, kufika kule, kesho yake usiku.

70 Nikasema, "Sasa, usiku wa jana ni upi?" Nikiisha kumalizia, karibu usingeweza kusikia, mnaona. Walikuwa tu kila mahali, kila dini na kadhalika. Nikasema, "Ni wangapi kati yenu sasa wanaotaka kumpokea Bwana Yesu Kristo?" Mnaona. Na kila kitu ambacho kingeweza kuonekana, kilimkubali Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi, kila mahali. Na—na,

bila shaka, usingeweza . . . Ambapo ningeweza kuona, kwani sikuweza kuona sana.

71 Tu—tusingeweza kufanya mkutano wa nje, mvua ikinyesha, na mambo kama hayo. Na watu tu huko wala usingeweza kuwafikia. Na, loo, lilikuwa ni jambo la kuhuzunisha sana ulilopata kuona. Na—nao wangali wakija barabarani na kadhalika, wakimkokota mbuzi mzee, mwajua, ama kitu kingine kama hicho, wakijaribu kufika mikutanoni.

72 Na kisha usiku wakati yule kipofu, nikasema, "Sasa ni yupi kati ya miungu wenu awezaye kuyafumbua macho yake?" Nikasema, "Huyu hapa mmoja wa waabuduo wenu wenyewe, ingawa ushirikina, umeyapofusha macho yake, akilitazama jua." Nikasema, "Anaabudu jua kwa sababu anajua ni kiumbe fulani kilichoumbwa, ambacho kimeumbwa, kiumbe fulani ambacho kimeumbwa, kitu fulani."

73 Lakini, nikasema, "Muumba mwenyewe aliyeliumba jua, aliumba macho ndani ya mtu huyu; mnaona, Yeye yule." Nami nikasema, "Sasa, akipenda, Mungu atayafungua macho yake; kabla sijawauliza tena, ni wangapi kati yenu watamkubali Bwana Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu, aliyesulubiwa?"

74 Wasingeweza kuelewa jinsi ambavyo Mtu huyo mtakatifu angeweza, akiwa vile tusemavyo, Mkristo asemavyo, angekufa. Nikasema, "Sababu iliyomfanya afe ilikuwa ni kuzichukua dhambi zetu." Nikasema, "Yeye hakuwa Nafsi ya tatu, ama Nafsi ya pili. Alikuwa ni Mtu yule yule, aliyefanyika mwili ili kuzichukua dhambi zetu." Nikasema, "Yeye, ilimbidi aje na kutengeneza . . . "

75 Nami nikawapa ile hadithi ndogo niliyohubiri hapa, usiku mmoja kabla sijaondoka, ya nyuki, mwajua, jinsi anavyouma, kisha anaacha mwiba wake, mwajua, wala hawezi kuuma tena. Basi ilibidi kuwa mwili wa mwanadamu, ili—ili nyuki wa mauti apate kuuma, kwa sababu mauti haimo ndani ya nafsi. Mauti iko katika ro-, . . . katika mwili. Hivyo ilibidi . . . Ilibidi Mungu afanyike mwili, apate kuondoa uchungu wa mauti. Na hivyo basi wakati . . . Hawana budi kuona hilo, mwajua, kwa sababu kuna wadudu wengi sana India, nao walikuwa—walikuwa . . .

76 Nikasema, "Sasa angalieni. Mungu anaweza, Muumba mwenyewe . . . Mtu huyu, katika ushirikina wake, akilitazama jua, akijaribu kupata rehema kwa nafsi yake, kwa maana anajua ya kwamba atakapokufa hana budi kwenda mahali fulani, kutoka hapa." Nikasema, "Ingawa pale, macho yake yamepofuka; na kwa kutokujua alifanya hivi. Lakini Muumba mwenyewe ambaye aliumba jua ambalo alilitazama, anaweza kumrudishia uwezo wa kuona katika macho yake."

77 Nikasema, "Je, ungekuwa tayari, bwana, kumpokea Bwana Yesu Kristo kama Mwokozi wako, nawe utaacha sanamu zote na chochote kile, na utamtumikia Yeye maadamu ungali hai? Kama

utafanya hivyo, inua mikono yako." Ndipo maskini jamaa huyo akainua mikono yake iliyokuwa ikitetemeka. Kila kitu huko huvaa tu kipande cha kitambaa kiunoni, mwajua. Naye akainua mikono yake, kwamba angefanya hivyo.

78 Nao kamwe hawaketi chini wanapokuwa kanisani. Kamwe. . .Kamwe hawana viti au chochote. Wanalala tu, ama kuketi chini, ama kuanguka chini, ama kulundikana mmoja juu ya mwingine, chochote wawezacho. Unaweza kuwazia jinsi ingekuwa. Kadiri tu uwezavyo kuona, wajua, watu wako hivyo.

79 Na hivyo nikamwomba Bwana mwema ayafungue macho yake. Na hapo, kwa neema ya Mungu, mtu huyo kipofu kabisa, machozi yakaanza kutiririka kwenye uso wake wenye makunyanzi na ndevuni mwake, mwajua, ndevu nyeupe, yakitiririka namna hiyo. Naye akaanza kusema jambo kwa sauti kuu katika lugha yake mwenyewe. Ndipo kila mtu akaanza kupiga mayowe. Naye huyu hapa akipitia kule, akimpigapiga kila mtu namna hiyo. Aliweza kuona, mtu aliyekuwa kipofu.

80 Sasa, Ndugu Cox na hao wengine, nafikiri, ameketi huko nyuma. Anaweza kuwaonyesha barua za thibitisho, la mambo haya iliyotoka India, na ingechukua muda mrefu, mrefu, mrefu.

81 Lakini vile tulivyoipanga, ni—nisingeweza kukaa. Ni. . .Sioni jinsi nilivyopata kukaa siku tano humo. Kama isingalikuwa ni kwa ajili ya mvulana wangu kule nyuma, Billy Paul, na msaada wa Mungu, kamwe sijui jinsi ningalifaulu. Billy alishikana nami. Na yeye—yeye akanipisha, akajaribu kunipisha. Nao hao watu, mnajua, ambao. . .Nao ni waoga sana. Hawataki kudhuru kitu, au chochote. Na inakubidi tu kuondoka, unaona, maana ungepondwa-pondwa chini ya huo umati, na sisi—sisi tusingejua, mwajua. Ungekanyagwa hata ufe. Unaona, huna budi kupitia humo.

82 Kwa hiyo, vema, nimerudi nyumbani tena, kwa neema ya Mungu. Ningeweza kusimulia mengi zaidi, lakini ni wakati wa shule ya Jumapili. Sitaki kuchukua mahubiri ya Neno katika hotuba ya umishenari.

83 Kifurushi chochote cha "msaada" ulicho nacho, na unataka kupokea ushauri, kitume India. Sina neno na Ujerumani; wao ni watu wazuri, ukiwalinganisha na watu hawa wengine. Lakini, ndugu, dada, tunawapelekea tu misaada wapate kujijenga, kisha tufanye vita vingine nao, mnaona. Hiyo ni kweli. Hebu tuipeleke mahali inakohitajika kweli, mnaona. Ikiwa una chochote cha kutuma, kitume India. Hao ndio wahitaji. Nao ni maskini, wasio na elimu; wana rasili mali, lakini hawana akili ya kujua jinsi ya kuikuza. Kitu pekee wanachojua ni kuombaomba, na hivyo ndivyo wanavyofanya.

84 Basi walikuwa wakitaka kunipeleka. . .Mnajua jinsi ninavyopenda kuwinda. Walikuwa wakitaka kunipeleka kwenye mawindo makubwa ya kuwinda simba marara huko juu

Bengal, wayagharamie. Nikasema, "Kwa hisani yenu. Chukueni pesa zile zile ambazo mngetumia kwake, mkawalishe hao watu maskini huko nje. Nitaenda nyumbani bila hiyo, mnaona. Hiyo ni kweli, kwa sababu na—naweza kuwinda mahali pengine, mnaona."

85 Ikiwa una nguo zozote kuukuu, chochote unachotaka kutuma kule, kipeleke India. Unaona? Karibu nimesafiri kote ulimwenguni sasa, na mi—mi—mimi ninajua ninachozungumzia. Na, kama ndugu Mkristo, India ina uhitaji.

86 Sasa, nimekuja nyumbani, nilitimiza kila kitu ambacho Bwana aliniambia nifanye, nijuavyo mimi, kadiri nijuavyo. Juma hili lijalo, nitawaambia jambo dogo lililotukia.

87 Nilikuwa nikila chakula cha jioni na gavana. Walikuwa wanipe wali wa kale pale, uliopikwa pamoja na miguu ya kondoo, na kukolezwa kwa mafuta ya zeituni. Mnaweza kuwazia, hauna ladha kabisa. Mimi. . . ulinifanya nichefuke sana karibu nisingeweza kuustahimili. Nusura nitapike. Huyo gavana akaangalia huku na kusema, "Bwana, naamini wewe ni mgonjwa."

88 Nami nikasema, "Loo," nikasema, "kidogo nafikiri hiki chakula ni tofauti."

89 Tulipofika hotelini, kulikuwako na daktari wa kibinafsi wa gavana pale, akinisubiri. Kasema, "Nataka kukuchunguza." Kasema, "Mimi ni daktari wa kibinafsi wa gavana.

Nikasema, "Loo, niko sawa."

90 Na kwa hiyo akaanza, bila shaka, kama muungwana, kweli, akaanza kunichunguza mwili wote. Naye akasema, "Nafikiri uko sawa." Kila kitu kilienda sawa hadi alipopima shinikizo langu la damu. Akaniangalia tena, kasema, "Hivi si umechoka sana?"

91 Nikasema, "Naam, bwana." Nikaanza kumwambia athari za hiyo mikutano, hayo maono, mwajua, kuingia kwenye hayo.

92 Kasema, "Sielewi jinsi ulivyo hai." Kasema, "Sitaki kukutisha, lakini," kasema, "shinikizo lako la damu liko chini kabisa." Akasema, "Mishipa yako ni dhaifu sana, hata haitasukuma damu yako mwilini." Mnaona? Kasema, "Shinikizo lako la damu liko chini kabisa." Kasema, "Utakuwa hapa muda gani?"

Nikasema, "Loo, nina mikutano miwili zaidi."

93 Akasema, "Vema, nakushauri urudi Marekani haraka iwezekanavyo, na umwendee daktari mzuri sana akuchunguze," akasema, "kwa sababu ningekushauri usiwe na mikutano yoyote kwa muda." Mnaona? Nikamwambia jinsi hiyo ilivyokuwa. Bila shaka, aliviita "viwango," mwajua, kupasua kutoka kimoja hadi kingine.

94 Nikasema, "Vema, bwana, nitakapoenda nyumbani," nikasema, "Nimewaahidi Wamarekani kwamba, nilikuwa nimewapa mikutano, tangu sasa na kuendelea haitakuwa hivyo." Nikasema, "Wao . . . Ningewaombea tu watu." Mnaona?

95 Na, maana, ninaona ha—haina matokeo kama inavyopaswa. Ninamwangalia ndugu yangu, Oral Roberts, na baadhi ya jamaa hao kule, ambao wana mikutano, na hata wanapata watu wengi zaidi wanaookoka, hapa Marekani, kuliko mimi. Ni kitu ambacho ninaamini kuwa nimekitumia vibaya, karama kuu ya Kiungu, ya karama ya unabii, na kuitumia kwa njia ya uponyaji wa Kiungu. Wala sidhani kama imemtia Mungu moyo, au kumfanya Mungu anipende sana, kwa kufanya hivyo, kwa sababu haingekuwa na matokeo mazuri sana.

96 Hakuniambia kuhusu watu hao, mwajua. Alisema hilo lilifanywa mara moja. Alimwakilisha hata Musa, kwa njia iyo hiyo. Musa alishuka kwenda Misri na kufanya miujiza yake, wakati mmoja. Hiyo ilitosha. Akaushika mkono wake, naye akaponywa ukoma; na kugeuza fimbo ikawa nyoka, na kurudi kuwa fimbo, na hilo likatosha milele.

97 Nami nafikiri, baada ya miaka kumi ya kuvuka Marekani, huku na huko, na kuchambua kila mji, watu wanaelewa ya kwamba ni Kweli sasa, mnaona. Wakati huu, ni kuwaombea watu, na hilo ndilo ninalokusudia kufanya.

98 Nimekuwa ninii sana—nimekuwa mzuri sana. Mnajua ninawapenda ninyi watu. Nami ninawapenda kwa upendo usiokufa, na Mungu anajua hilo. Ilibidi nijitenge. Kunao watu, kote humu—humu Marekani, ambao ningependa kupeana mikono nao, nami nimetamani kufanya hivyo katika mikutano. Nisingeweza, mnaona. Hujui athari hilo ono liliyo nayo kwako. Mara tu unaposimama mbele ya huyo mtu, hilo hapo, unaona. Nami nisingewaambia watu jambo hilo wakati mwingine, lakini hilo hapo mbele ya huyo mtu. Niligundua mambo, ya watu, laiti nisingaliyajua. Watu ambao watakuwa marafiki zangu, na hata hivyo, ungejua kwamba haikuwa sawa. Mungu angeshuka sasa na kuniruhusu, ningeweza kuwaambia mambo ambayo yangewashangaza.

99 Na hapo nimemwomba Roho Mtakatifu, kama akipenda, ambapo ameniambia . . . Nimemwomba kama angeniruhusu kwanza nirudi tena nitulie kufikia mahali nilipokuwa nilipoondoka humu maskanini. Nirudi tu pale, na anijalie kutulia, mpaka, nitakaposimama mbele ya watu, haitakuwa ono. Itakuwa naweza kuzungumza na ndugu pasipo kuona hali yake. Papo hapo nimwombee tu, mnaona, na kuwa kama . . . Nimemwomba Mungu afanye hivyo.

100 Nimekuja nyumbani. Nami ninajua, juma hili, kwamba hakuna mtu ambaye amekuwa hapa kwenye nyumba. Ni jambo jema. Nimekuwa huko kama siku tano, nisingeweza

hata kusogea. Ni—nimekuwa mahali, ningeinuka, inaonekana kama kwamba mifupa yangu inauma, na kila kitu. Bila shaka, mabadiliko hayo huku, saa kumi na moja na nusu kamili, tofauti, kati ya Bombay na hapa. Sasa hivi ni karibu tu wakati wa mimi, loo, ni—ningekuwa nimelala saa moja ama mbili zilizopita, mnaona; kwa hivyo ni usiku, na imebadilika tu. Halafu hilo shinikizo dhaifu la damu lilikuwa limeshuka chini namna hiyo, nami nisingeweza tu kuamka na kuketi. Hivyo tu. Nilijiletea mwenyewe, nikijaribu kufanya kazi kupita kiasi. Kwa hiyo, sasa, nimerudi nyumbani, kwa neema ya Mungu.

101 Na sasa, juma hili lijalo, nitaondoka, nikae tu kwa muda, majuma mawili ama matatu, peke yangu; kukaa peke yangu, kuomba, kwanza. Nitaenda kuwinda, Bwana akipenda. Lakini kabla sijafanya hivyo, itakuwa, ninaenda siku chache kabla ya majira na kadhalika. Ninaenda Colorado. Ninataka kukaa angalau wiki mbili au tatu, au labda zaidi, kuwa tu peke yangu na upweke wangu, na kusema, "Mungu, mimi hapa."

102 Huenda nikashuka na kumwomba Bw. Mishler kazi tena, Bw. Mishler, narudi kwenye Kampuni ya Utumishi wa Umma.

103 Nime—nimetimiza kile alichoniambia nifanye. Nami ninasimama Maskanini, asubuhi ya leo, jinsi tu nilivyoondoka miaka kumi iliyopita. Sina meneja. Meneja wangu alijiuzulu wakati magumu yalipoingia. Sina meneja yeyote.

104 Mvulana wangu anaondoka. Na mvulana wangu, anayeketi kule nyuma, anaenda Jeshini. Amekuwa rafiki msiri wangu. Alishikana nami.

105 Baadhi yao sikuzote walinigombeza, "Kwa nini unafuatana na Billy?"

106 Laiti ungalijua jinsi nilivyombeba mvulana huyo mkononi mwangu alipokuwa kitoto kichanga cha kunyonya, bila mama. Niliweka chupa yake chini ya kichwa changu usiku, bila moto ndani ya nyumba wa kutia joto chupa yake, na kumlisha. Amekuwa rafiki msiri wangu, muda wote. Tutakufa hivyo, Mungu akipenda.

107 Pengine ataenda Jeshini mara moja; alipata makaratasi jana kufanya uamuzi wake, kama anataka kujitolea au—au kuitwa jeshini. Naam, sitakuwa naye.

108 Ndipo basi ni—niko peke yangu, lakini si peke yangu, mnaona. Yuko Mmoja aliyenitoa kwa mama yangu, ambaye amenilisha, ambaye amenivusha kwenye majaribu haya mazito. Neema Yake imenileta salama umbali huu. Ninaamini Hiyo itanivusha. Nami nimefika mahali ambapo nina . . .

109 Ninataka kuliomba kanisa jambo moja zaidi kabla hatujafikia mahali pa kujifunza Maandiko, yaani, kwamba mniombee. Nimepatwa na roho ya ukosoaji, na inanisumbua. Nilimwambia mke wangu, jana, mara ya kwanza. Jambo

fulani lilitendeka sasa, nami nilikuwa nimeketi kwenye uga, nikamwambia. Alikuwa amenikumbusha, nami nikamwambia kuhusu hilo. Nikasema, “Mpenzi, nimefika mahali ambapo nawakosoa watu.” Sitaki kuwa . . . Ni—ni kazi ya nani? Si yangu. Naye Mungu Ndiye wa kukosoa, si mimi.

110 Kulikuwa na mwanamke, aliyeenda kule, Bibi Dowd. Sijui kama mmewahi kusikia habari zake au la. Loo, aibu kubwa sana iliyokuwa India! Hiyo ndiyo sababu tusingeweza hata kufanya mikutano yetu hadharani. Alifika kule na kujaribu kuchukua sadaka kutoka kwa watu hao. Na—na—na kwa sababu wasingetoa maskini rupia zao . . .

111 Maskini mwanamke aliye na kazi, akibeba mota kichwani mwake, kupanda vipandio na mambo kama hayo, kuanzia saa kumi na moja hadi saa nne, hupata rupia moja kwa siku, senti ishirini na moja, mnaona. Anapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kudumisha kazi hiyo. Mwanamke anayetembea kwenye matope yaliyomfikia magotini mwao, na kadhalika, maskini jamaa hao wadogo, wanawashughulikia watoto wao wachanga na kadhalika; rupia moja, senti ishirini na moja.

112 Naye huko akiwagombeza hao watu, na kuchukua rupia hizo na kuzigeuza kuwa pesa za Marekani! Nao wakasema, “Mlikuja kuchukua tulicho nacho, sio kutusaidia.” Mnaona, “nyinyi watu”!

113 Hawakuhitaji kunipa hata senti moja, kwenda kule wala kurudi, kulipia gharama zangu, kulipa kodi zote za ukumbi, bili zote za hotelini, kila kitu. Halafu kila kitu nilichokuwa nimebakisha, nilikichukua mtaani, sio kuyapa mashirika fulani. Nilikichukua na kuwapa hao maskini ambao wanakufa kwa njaa. Hapo ndipo pesa zenu zilienda. Hapo ndipo pesa zenu zilienda. Hiyo ni kweli kabisa, nijuavyo mimi, ningeweza kulifanya hilo mwenyewe. Laiti ningelikuwa na nyingi zaidi, kulifanya nazo.

114 Sasa, lakini, sasa, ndugu yangu, dada, mwanamke huyu alianza kuchukua sadaka, na kuwagombeza. Wakasema, “Mlikuja kuchukua tulicho nacho, si kutusaidia. Nilidhani mlikuja kutusaidia.” Alidhaniwa kuwa mponyaji wa Kiungu.

115 Alinikasirikia, nilipokuwa Pwani ya Magharibi. “Howard,” akasema, “Nataka kumwona baba yako.” Alikuwa ameolewa na mwanamume fulani kutoka kule Misri, ama chochote kile. Kasema, “Ninaenda India, pia.”

116 Kasema, “Vema, bibie, wakati huo upako ukiwa juu yake, sisi . . . watu kamwe hawamkaribii.”

117 Kasema, akasema, “Wewe mwambie kuwa mimi ni Bibi Dowd!” Kisha kasema, “Nikimtangulia kwenda India, nitadhibiti hali ya mambo kabla hajafika huko.” Kasema, “Mikutano yangu ni mikubwa kuliko aliyowahi kuwa nayo,

kwa vyovyote vile." Vema, hiyo ni kweli, huenda ikawa, unaona. Sijui.

118 Lakini kuwazia, alikuwa ameyadhibiti mambo, kufikia mahali ambapo hata usingeweza kufanya mkutano hadharani. Ndivyo ilivyokuwa. Na wao—wao wakaanzisha fujo, ndipo akasimama pale na kusema, "Enyi mashetani weusi, ninyi!" Akaendelea kusema hivyo. Nao wakajaribu kumfukuza, wala asingeondoka. Ndipo mtu mmoja akampiga kichwani kwa tofali, ndipo wakambeba na kumwondoa. Kwa hiyo wao, basi, wakamtoa nchini haraka. Akashuka kwenda nchi nyingine kule, ikambidi Baron von Blomberg kushuka kwenda kumwona mfalme, na kadhalika, ili kumwondoa huko, kujiepusha na mauaji ya umma. Hivyo basi, hivyo wao. . .Hiyo hapo, nami ninaangalia hilo na kulikosoa hilo.

119 Nikarudi, na kitu cha kwanza kilichowekwa mikononi mwangu kilikuwa ni Sauti ya Uponyaji, nami nikaona mkutano huu wa A. A. Allen na kuona jinsi usivyo wa kimaandiko. Ndipo basi nikaukosoa, mnaona, "Loo, jamani," nafikiri. Lakini hebu waangalieni hao watu maskini, watu wazuri sana, wako huko nje wakifuata hayo, mnaona, wakienda pamoja naye, na watu wanyoofu wa moyo.

120 Ninaangalia huku na huko na kuona mambo haya mengine yanayoendelea, na katika hayo ni—ninaanza kuyakosoa moyoni mwangu, mnaona. Wala sitaki kuwa hivyo. Nikifanya hivyo, nitapoteza kibali kwa Mungu. Mnaona? Basi jambo pekee. . .

121 Nami nawatazama Wamarekani na kuona jinsi; nawaangalia wanawake, jinsi wanavyovalia; na kumwangalia mwanamume; jinsi wanavyofanya; na jinsi wanavyokunywa pombe, na kutukana, na kuvuta sigara, na kutafuna tumbaku, na kudai kuwa Wakristo, mpaka inanichefua kabisa. Ninapoona kile upande huo mwingine ulicho, na kuona hili; kisha naangalia katikati, nawazia, "Ee Mungu!" Lakini sikilizeni hili, kwani ni vita vya nani? Mungu alisema, "Acha magugu na ngano zikue pamoja. Malaika watakuja na kuwatenganisha mwishoni mwa wakati." Sio mimi.

122 Kwa hiyo nisaidie, ninaposimama hapa, mkono wangu umeinuliwa, mimbarani, unisaidie nisimkosoe mtu yeyote. Na unisaidie, ili Mungu anipe roho moyoni mwangu, kwamba, badala ya kukosoa, nitawapenda, kwa vyovyote vile, na kuendelea.

123 Imekuwa kila mara ni kujitahidi, na kujitahidi, na kujitahidi. Mpaka, mimi ni binadamu tu. Nguvu zangu za akili zinavunjika namna hiyo, mnaona. Nami sina budi kuondoka, nipate kupumzika kidogo.

124 Na hiyo ndiyo sababu ninaondoka, nikakae peke yangu, kuomba kwamba Mungu ataniondolea hisia hiyo ya ukosoaji, na kuniyeyusha kabisa. Sasa, ningeweza kwenda na kutenda

hivyo, lakini hilo lisingetoka moyoni mwangu. Nami ningekuwa mnafiki basi, kweli kabisa, mnaona. Nataka litoke moyoni mwangu, kwamba kweli ninawapenda wale wasiopendeka. Hilo Yesu alifanya. Nilipokuwa mkosoaji, nilipohitaji kukosolewa, na bado, Yeye angali ananipenda, hata hivyo. Basi hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Ninyi niombeeni.

125 Natumaini kuwaona tena, yapata Novemba, labda nirudi na kufanya uamsho hapa maskanini kabla ya sisi . . .

126 Kwa hiyo, sasa, hili hapa jambo moja ambalo nimefanya, nimeuliza hili. Jambo moja zaidi. Nimeninii . . . sitaki kuwahudumia wagonjwa, si zaidi ya kutumia tu leso, ama kadhalika. Ninajaribu kuliondokea hilo ono, mnaona. Na hasa sana kadiri nilivyo dhaifu sasa, na kwenda kusimama mbele ya watu, vema, ndipo ukianza hilo, ono hilo linarudi. Ninataka kuondoka na kujituliza kufikia ambapo naweza kuja huku na kufanya mkutano tofauti. Mtaniombea, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na, basi, na mimi—nami ninaomba, katika—katika barua, na kutuma leso na kadhalika kwa wagonjwa na wanaoteseka—wanaoteseka.

127 Lakini watu wanaponipigia simu waombewe, ninawaelekeza kwa Ndugu Neville, ama baadhi ya hao wengine, waende wakaombe.

128 Maana, ninaposimama mbele ya mtu, hilo linanitikisa likanirudisha moja kwa moja kwake tena, mnaona. Nami ninataka kuliondokea, ili nipate kulala chini, niseme, "Sasa, Bwana, kwa mapenzi Yako tu. Wakati wowote unapotaka nijue chochote, unijulishe. Nami nitaliweka siri kwangu, isipokuwa uniambie niliseme." Mnaona ninachomaanisha? Halafu niende kule na kuwaombea wagonjwa, na kubadilisha huduma yangu kwa jumla. Ninaweza kuwa na mikutano mirefu zaidi, mikutano bora zaidi, na kila kitu kingine nilichokuwa nacho, kuliko nilivyoweza hapo awali.

Bwana awabariki sasa, tunapoinamisha kichwa chetu.

129 Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe, asubuhi ya leo, kwa wakati wa kuzungumza juu ya misheni, na jinsi ambavyo umetubariki na kutusaidia. Na ni mara ngapi nimewazia, wakati mawimbi yalikuwa yametanda, na majaribu makubwa yalikuwa yanaendelea, kweli ningerudi nyumbani tena. Lakini, hapa, mimi hapa tena. Bwana, sikuzote Wewe hunirudisha. Ninakushukuru kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya mchungaji wake, kwa ajili ya watu wake. Utubariki.

130 Na sasa, Baba, asubuhi ya leo, mimi . . . moyo wangu unatazama ng'ambo huko India, na kuwaza, wamelala huko nje mtaani, asubuhi ya leo. Kote huko chini kando ya ufuo huo, chini kwenye hivyo vibanda vidogo vya kale, huko chini, maskini hao watu fukara, wanaokufa kwa njaa, wasio na elimu; wasiomjua Bwana Yesu, wakiabudu aina fulani ya ushirikina au sanamu.

Basi, Baba, jinsi ninavyoshukuru kujua ya kwamba umenijalia kukujua Wewe; kujua, ni Uzima.

131 Sasa ninaomba ya kwamba utanisaidia. Ondoa roho ya ukosoaji kutoka kwa mtumishi Wako, Bwana. Mungu, sitaki kuninii. . .Ikiwa hao watu wamekosea, Wewe uwe mwamuzi, Bwana. Nijalie nipende tu, kwa vyovyote vile. Sivyo, Baba? Wanawake wakivalia vibaya, na kujitumia vibaya na kuwa makahaba, nalo taifa letu lizame, ninawezaje kubadilisha historia wakati Wewe umelinena, Bwana? Lakini ninaomba ya kwamba utanisaidia tu, na unijalie kuwa mwenye upendo na fadhili, nipate kuwa mtumishi Wako na kufanya mapenzi Yako. Mambo haya ninaomba, Baba, kwa ajili ya utukufu Wako.

132 Sasa tubariki. Na kwa kuwa nimeombwa kufundisha Neno, kidogo. Baba, tupe tu ujumbe mfupi sasa, ili Neno lipate kuenea, ipate kuwa siku kuu kwetu. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

133 Vema. Sasa nina dakika kumi na tano ifike saa tano. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, tunaweza kuchukua kama dakika thelathini na tano? Hiyo itakuwa sawa, nasi tutoke kama saa tano na nusu? ["Amina."] Sasa tunaenda wapi?

134 Nilikuwa nimeketi hapa, nikiwazia kuhusu kufundisha kutoka kwenye Agano la Kale. Lakini, wewe, kwa kawaida mimi huninii tu. . .Unaingia katika Agano la Kale wakati wote. Kwa hivyo mtu fulani alisema, "Ndugu Branham, kwani hujui lolote ila Agano la Kale?" Vema, ni zuri. Nitakapojifunza hilo, basi nitajifunza hilo Jipya. Lakini unapojifunza moja, unajifunza yote mawili. Unaona, yote mawili yako pamoja.

135 Lakini hebu tufungue Agano Jipya, mahali fulani. Sijui ninyi nyote mmekuwa mkisoma wapi, au chochote kile. Hebu. . . Nawaambia, hebu tumsikie Yohana Mtakatifu. Hebu turudi kwenye Yohana Mtakatifu wa kwanza, na tuanze kusoma Yohana Mtakatifu. Sasa hiyo ni ninii tu. . .Ninaifungua tu. Sijui. Kwa hivyo tutaanza tu kusoma katika Yohana Mtakatifu. Hilo ni sawa kwa kila mtu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ndivyo? Vema, Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza.

136 Na sasa, labda, Jumatano hii ijayo usiku, nilisikia. . .Nataka kuwa pamoja nanyi usiku wa leo. Nataka kushuka na—na kuwa pamoja nanyi usiku wa leo, na halafu Jumatano usiku, pia. Nafikiri kwamba hatutaondoka kabla ya Jumatano, kwa hiyo nitakuwa hapa Jumatano usiku. Nina hakika kabisa itakuwa Alhamisi ijayo au Ijumaa, mojawapo, kabla hatujaondoka. Kwa hiyo basi nitakuwa hapa Jumatano usiku, Bwana akipenda, kwa ajili ya ibada. Na sasa tunataka ku—kufundisha kidogo, labda, Jumatano usiku, Bwana akipenda.

137 Aisee, Ndugu Fleeman, hilo ni wazo zuri, vua tu koti lako sasa na ujisikie uko nyumbani.

138 Kuna mtu yeyote aliye na neno dhidi ya mtu yeyote? Kama unalo, inua mkono wako na uwaendee. Sasa, hebu na tuifanye tu karamu hii moja kubwa ya kale ya upendo, asubuhi ya leo. Mwasemaje? Kila mtu, na chochote ulicho nacho, ikiwa mtu huyo hayupo hapa, hebu tuseme, "Bwana Yesu . . ." Hebu tuliweke chini ya Damu sasa hivi, na, tangu siku hii na kuendelea, "Sitaliwazia tena." Hebu twendeni tu, na mwache kila kitu kianze upya sasa.

139 Loo, laiti ungejua tu jinsi—jinsi unavyopaswa kuwa na furaha. Katika dini zote za ulimwengu, kuziona, kila moja, hazina msingi kabisa. Na ni moja tu iliyo halisi, hiyo ni Injili ya Bwana Yesu Kristo. Haidhuru, kama inatoka kwa kanisa la Methodisti, kanisa la Baptisti, kanisa la Presbiteri, Bwana Yesu Kristo ni wa kweli. Amina. Mnaona, haidhuru inatoka wapi, Ukristo unang'aa zaidi. Ndicho kitu cha pekee kilicho na msingi, kabisa. Mambo mengine . . . Dhabihu ya Damu ya Bwana Yesu Kristo ndiyo tumaini pekee la ulimwengu.

140 Sasa, nimeona dini zao. Nimeona sanamu zao. Nimeona ushirikina wao. Nimeona miungu yao na wote, na kila . . . Nimezisoma, na kusoma Ku—Kurani, kwa kila kitu ninachojua kusoma. Na jinsi hizo, kila hali, na zinakuwa ushirikina. Nalo linakufanya tu uthamini, ni halisi sana, loo, ya kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ndiye tumaini pekee la ulimwengu. Naye Ndiye pekee aliyewahi kufufuka katika wafu. Nasi tunaweza kuthibitisha ya kwamba Yeye alifufuka katika wafu, Naye anaishi leo. Amina. Loo, jamani, Ndugu Neville! Hujui jinsi nilivyo na furaha kuwa Mkristo! Loo, unapaswa kuwa na furaha sana!

141 Sasa Injili hii kuu ya Yohana Mtakatifu hapa, kulingana na Yohana Mtakatifu. Yohana alikuwa mpendwa. Tunaamini huyu Yohana Mtakatifu alikuwa ndiye yu—yule mpendwa aliyeegemea kifuani mwa Yesu, na—na kadhalika. Aliishi hadi kuwa mtume mkongwe kuliko wote, au aliishi muda mrefu kuliko hao wengine wote. Na yeye—yeye . . .

142 Petro alisulubiwa kichwa chini, miguu yake juu. Andrea alisulubiwa mikono kando, *hivi*, na kupigiliwa misumari. Niliona kule chini ambako walimkata kichwa Paulo Mtakatifu, kule Rumi.

143 Aisee, ninayo mengine, loo, ni—nitajaribu kuleta hilo wakati mwingine nitakapokuja, picha za ufia imani huo wote na kila kitu, na kuwalisha simba, na kadhalika. Ninayo folda yote kubwa. Nitashuka nazo, na kutundika moja kwenye mlingoti mmoja, na nyingine kwenye mwingine, kadhalika, ili uweze kuziona na kuzichunguza, zote katika Kiingereza.

144 Angalieni, loo, ni tamasha la kuvunja moyo jinsi gani, ambapo walikikata kichwa cha Paulo pale, na kumtupa nje katika mfereji wa maji machafu, na kumwacha . . . nikawaza,

loo, jamani, mara shoka lilipokigusa kichwa chake tu alikuwa Utukufuni. Amina. Si ajabu, alisimama pale kwenye seli ile, alipoandika, "Ewe mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Aliandika, akasema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri. Mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. Tangu sasa iko taji ya haki iliyowekwa kwa ajili yangu; ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki atanipa Siku ile." Loo! Mbona, inakufanya ufikirie.

> Maisha ya watu mashuhuri yote yanatukumbusha
> Na tunaweza kufanya maisha yetu adhimu,
> Lakini kuachana huacha nyuma yetu
> Kumbukumbu za kudumu.

145 Sasa, Yohana, yule mfunuzi mpendwa. Na, Yohana, kuna akina Yohana kadhaa hapa katika Biblia. Lakini yule Yohana, Yohana Mtakatifu, yule tunayemzungumzia asubuhi ya leo, mtume wa Bwana Yesu Kristo, mmishenari aliyetumwa na Mungu.

146 *Mmishenari* ni "mtu aliyetumwa." Mara nyingi nimeshangaa jinsi watu wanavyosema leo, "Loo, kuna mitume kumi na wawili tu, mnaona, kumi na wawili tu." Mmesikia hayo. Vema, neno lenyewe linamaanisha, "mtu aliyetumwa."

147 Paulo hakuwa mtume kulingana na wale kumi na wawili. Lakini hivi mmetambua, walimchagua Mathiya, naamini ndivyo, ama Mathiya, kupachukua mahali pa Yuda. Na hivyo ndivyo mwanadamu alivyofanya. Yeye. . .husikii habari zake tena. Lakini Mungu alimchagua Paulo kupachukua mahali pake, mnaona. Basi angalieni yale Paulo aliyofanya! Mnaona, inaonyesha tofauti kati ya kuchagua kwa mwanadamu, na kuchagua kwa Mungu. Na hiyo inafanya. . .inanipa neema nyingi moyoni mwangu kwa mambo na makosa, na kadhalika.

148 Nimesikiliza, dakika chache tu zilizopita, kwenye redio, huyu Dk. DeHaan maarufu, mwalimu wa ajabu, jamani, ndugu mpendwa. Nampenda kwa moyo wangu wote; Mungu anajua hilo. Ili kuona tu jinsi watu mashuhuri wanavyoweza kufanya makosa! Ndipo nikawazia, punde tu, ndugu, nilipoliona kosa alilokuwa akifanya, niliwaza, "Mungu, nitafanya mambo yale yale, pengine, kwa hiyo yaangalie yangu."

149 Dk. DeHaan alisema, "Ubatizo ulikuwa ni wa wakati mmoja tu katika Biblia." Nimesikiliza tu hivi punde nikija humu kanisani asubuhi ya leo. Kasema, "Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulimbatiza kila mmoja wa mitume, ukawazamisha mle chumbani. Nasi tunabatizwa kwa maji, kuuwakilisha huo. Na huo ulikuwa ndio wakati pekee ambao waliwahi kubatizwa na Roho Mtakatifu. Mara moja tu, katika Biblia."

Nikawazia, "Loo, Dk. DeHaan!"

150 Mbona, yapata siku kumi baadaye, Filipo alishuka na kuwahubiria Wasamaria. Akawabatiza katika Jina la Bwana Yesu, ila tu Roho Mtakatifu alikuwa hajawajilia bado. Petro akashuka na kuweka mikono juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

151 Karibu miezi miwili, au miezi mitatu, baada ya hapo, Petro alikuwa juu ya paa, naye akaona ono, akapanda akaingia . . . hadi nyumbani mwa Kornelio. Na wote walikuwa wamesimama pale, nao walikuwa na moyo mmoja, huku wakiomba. "Basi Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia, kama alivyofanya hapo mwanzo." Nao walikuwa hata hawajabatizwa kwa maji, bado. Akasema, "Ni nani awezaye kuzuia maji, kwa kuwa hawa hawajabatizwa; watu waliompokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi hapo mwanzo?" Kwa hivyo mwili mmoja mdogo hapo uliwakilishaje . . . Loo, la, la.

152 Yapata miaka kadhaa baadaye, kama miaka ishirini baadaye, ilimbidi Paulo apite kati ya nchi za juu za Efeso, unakutana na wanafunzi fulani. Akawaambia, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

153 Wakasema, "Hata hatujui kama kuna Roho Mtakatifu."

154 Akasema, "Mmebatizwa? Mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

Wakasema, "Wa Yohana."

155 Kasema, "Lakini Yohana alibatiza kwa toba, akisema kwamba mgemwamini Yeye atakayekuja, Bwana Yesu."

156 Waliposikia haya, wakabatizwa tena, kwa maji, katika Jina la Bwana Yesu. Na katika . . . Akaweka mikono juu yao, naye Roho Mtakatifu akaja juu yao pale, mnaona, njia ile ile kama alivyoshuka hapo mwanzo. Loo, naam! Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ubatizo wa maji, unaendelea moja kwa moja, na utakuwa mpaka Yesu atakapokuja tena.

157 Lakini ni kosa la jinsi gani, mnaona, ni kosa la jinsi gani, kwa mwanachuoni mkuu, mwenye akili namna hiyo! Inaonyesha, haijalishi una akili jinsi gani, unajua kiasi gani, wewe ni mwanadamu na utakosea, hakika kabisa. "Vita ni vya Bwana." Hiyo ni kweli.

158 Mimi huona mambo, hata katika maono na mambo ambayo Bwana amenionyesha, kisha nageuka moja kwa moja na kufanya vinginevyo. Mnawazia? Na Mungu akinionyesha! Nilikuwa nalo huko Lisbon. Nikasema, "Bwana, ondoa tu mkono Wako kwangu, hata sistahili kuwa mtumishi Wako." Kuona jambo aliloniambia, nami nilikuwa nimesahau yote juu yake, nikaenda moja kwa moja. Likatokea. Nikawazia, "Loo, jamani! Hapo, kwa nini sikukumbuka hilo." Mnaona? Hapa, nilikuwa nimeliandika, mfukoni mwangu hapa, kwenye kipande cha karatasi, ndipo nikaingia moja kwa moja na kufanya kitu vinginevyo. Mnaona?

Hapo, inaonyesha ni kiasi gani cha ninii...kiasi gani, jinsi nilivyo mzuri, mnaona, sio...Loo, mbaya kuliko hao wote, angekuwa ni mimi. Kwa maana, baada ya Mungu kukwambia ufanye jambo fulani, nawe unageuka moja kwa moja na kufanya vinginevyo, hilo ni baya sana. Unaona?

159 Kwa hiyo, unaona, haidhuru mtu huyo ni nani, yeye si kitu ila mwanadamu. Yeye, atafanya makosa. Kwa hivyo na tuvumiliane, na tufanye vizuri tuwezavyo. Hilo ndilo jambo pekee tunaloweza. Vema.

160 Yohana, sasa, kifungu cha kwanza. Kila mtu amefungua Biblia yake? "Hapo mwanzo..." Loo, aisee, hii ni nzuri, sivyo, ya kuanzia?

> *Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.* (Angalieni!)
>
> *Tangu mwanzo huyo alikuwa pamoja na Mungu.*

161 Aisee, hebu tuendelee hapa chini, kifungu cha 14. Nimefundisha juu ya hili mara nyingi sana, na kuliwazia. Tazama.

> *Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, (nasi tukauona utukufu wake, utukufu...wa mwana wa pekee atokaye kwa Baba), amejaa neema na kweli.* (Tazama!)
>
> *Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
>
> *Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu,...*

162 "Hapo mwanzo..." Sasa hebu tupate ninii halisi...Hapa, naona kitu. Naye Roho Mtakatifu hapana shaka aliamuru jambo hili liwe hivyo, mnaona. Naona jambo kubwa hapa. "Hapo mwanzo alikuwako Neno."

163 Sasa, huwezi kurudi nyuma zaidi, tukinena kiakili, kuliko hapo mwanzo. "Hapo mwanzo," kabla ulimwengu haujakuwapo, kabla hakujakuwapo nyota, kabla jua halijakuwapo, mwezi, chochote kile, kabla ya kuwepo na uumbaji wowote, hapo ndipo "hapo mwanzo." Hiyo ni kweli? Sasa, kadiri tuwezavyo kwenda, ni kurudi mwanzoni.

164 Na hapo mwanzo, Mungu alikuwako. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa Mungu, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Basi, Neno lilikuwa ni Yesu Kristo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jamani! Basi Yule aliyekuwa... "Hapo mwanzo alikuwako Yesu Kristo."

165 Basi, katika mawazo yetu ya Kikatoliki, ya "Uwana wa milele," isingewezekana. Kwa maana, kama Yeye alikuwa

Mwana wa Mungu, ilimbidi awe na mwanzo wa wakati. Alipaswa kuwa “aliyezaliwa na,” apate kuwa Mwana, (hiyo ni kweli?), kama Yeye alikuwa Mwana wa Mungu.

166 Loo, tutamalizia hapa katika Maandiko mazuri ya kale! Jinsi ninavyoyapenda sana! Ninii tu . . . Unajisikia uko nyumbani unapoyaingilia, mwajua. Je, hamyapendi?

167 “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Neno Lenyewe lilikuwa Mungu. “Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu; nasi tukamwona, katika utukufu wa Baba,” mnaona. Tuliliona Neno lililokuwako hapo mwanzo, likifanyika mwili hapa duniani. Sasa, ni jambo la ajabu jinsi gani, kuwazia ya kwamba Mungu, alifanyika mwili, kuondoa dhambi.

168 Sasa, kama tungeweza kupata ushirikina wa ulimwengu, jinsi wanavyoabudu na wanavyotaka kuwa wema. Sasa, baadhi ya madhehebu yao pale, ya dini zao potovu, wanawazia, “Mtu akiwa mzuri kweli, anakuwa mungu. Na, yeye, yeye ni mungu basi.” Nao wanamwabudu kama Mungu.

169 Halafu basi sababu nyingine wanamwabudia . . . Ni vigumu kufundishwa katika—katika kusanyiko lililochanganyikana kama hili. Kwa sababu, chembe zazi ya uhai hutoka kwa mume, mnaona, nao wanafikiri kwamba “uhai unakaa ndani yake, na Uzima wa Milele, uhai unaoendelea, ukipitia kwa mwanamume, kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine. Tumekuwa hapa sikuzote. Sikuzote tumekuwa. Roho yeye yule, akitenda kazi tena na tena, ndani ya watu, mnaona.” Na, hivyo basi, wanamwabudu huyo mtu kwa sababu kutoka kwake inakuja chembe zazi ya uhai.

170 Sasa, lakini, hapa inatwambia, ya kwamba, kabla hapajakuwapo na mtu. Kabla! “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa Mungu, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu. Naye, Neno, alifanyika mwili!” Sasa, kadiri tu akili ya mwanadamu inavyoweza kwenda, huo ndio umbali tunaoweza kurudi nyuma sasa, kufikia “hapo mwanzo.” Hiyo ni kweli? “Hapo mwanzo alikuwako Neno.” Lakini sasa huo ndio umbali tunaoweza kwenda kwa theolojia. Huo ndio umbali tunaoweza kwenda kwa akili zetu. Lakini ufunuo unatubeba ukatupeleka mbele ya hayo. Hiyo ni kweli?

171 Sasa, kama unafundisha jambo fulani juu ya theolojia, unawazia, “‘Hapo mwanzo alikuwako Neno,’ huyo alikuwa Mungu. ‘Naye Neno alikuwa Mungu,’ hiyo ni kweli. ‘Naye Neno yuyu huyu alifanyika mwili, akakaa kwetu,’ mnaona. ‘Na, basi, Mungu alifanyika mwili. Hilo halina ubishi,’ hiyo ni kweli. ‘Mungu alifanyika mwili.’ Tunaamini hilo.” Lakini, sasa, kabla ya *Huyu* kuwa Neno . . .

172 Neno ni nini? Neno ni dhihirisho la wazo, ni tamko la wazo. Je, hiyo ni kweli? Kabla ya kusema chochote, bila kujijua unaliwazia kabla hujalinena. Hiyo ni kweli?

173 Kwa hiyo, "Hapo mwanzo alikuwako Neno," huo ndio umbali tuwezao kurudi nyuma, kwa *Hili*, kwa theolojia. Lakini kabla Neno halijakuwako, lilikuwa ni wazo, nalo hilo wazo likadhihirishwa. Mnaona ninachomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

174 Sasa, hivyo ndivyo vile Yeye alivyosema. Kwanza, Yeye aliwazia, kisha akalinena hilo Neno, nalo Neno likadhihirishwa. Loo, jinsi Mungu asivyoweza kukosea! Angalieni, kila wazo, linaponenwa.

175 Wakati, Yesu, si ajabu, alipotoka mlimani usiku ule, na kuangalia ule mti, apate chakula, hapakuwapo na chakula kwenye huo mti. Naye akasema, "Mtu asile kutoka kwako." Naye akaendelea, akaenda zake. Kesho yake, akirudi, huo mti ulikuwa umenyauka. Nia ya Mungu; nia, ambayo, hapo mwanzo, hilo lilikuwa ni wazo kabla halijakuwa Neno, lililomdhihirisha Yesu Kristo, Yule yule alikuwa akilitamka Neno hilo tena. Mnaona?

176 Na kila Neno katika Biblia ni mawazo ya Mungu yanayokaa katika umbo la mbegu, ambayo yakipokelewa ndani ya mwanadamu, na kunenwa kwa wazo lile lile ambalo liliifanya Biblia kuwako, hulitimiza hilo jambo. Mnaona ninachomaanisha? Kanisa lingeweza kuwa na nguvu kiasi gani! Biblia ilisema, "Nia hii iliyokuwa ndani ya Kristo na iwe ndani yenu. Aonavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Sasa, mawazo yako, kama yakitamkwa!

177 Kama vile, Mungu alisema, "Ulimwengu na uwepo." Kabla halijaweza kuwa neno, ilibidi liwe wazo. Kwa hiyo, Mungu, katika uumbaji, aliumba ulimwengu kwa wazo Lake, kwanza, kisha akata-. . . akaunena. Nalo wazo, lilipotamkwa, likawa mwili. Mnaona ninachomaanisha?

178 Sasa, kama Roho yeye yule aliyesema, "Iwe Nuru," ikawa Nuru; aliyesema, "Miti na iwe," na kukawa na miti; na ikiwa nia iyo hiyo iliyokuwa ndani ya Kristo, iko ndani yenu, ni zaidi sana kiasi gani ingeweza kusema, "Kusiwe na kansa," nayo itaondoka; "Macho mapofu na yafunguliwe," na ingetimia! Mnaona? Ni, ni wazo lako. Yesu alisema, "Amin . . . "

Ulisema, "Huyo alikuwa ni Yesu."

179 Lakini ngoja kidogo. Alisema, "Mwamini Mungu. Kwa maana, amin, amin, nawaambia, kama utauambia mlima huu, 'Ng'oka, ung'olewe ukatupwe baharini,' wala usiwe na shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba kile unachosema kitatimia, kitakuwa chako kile ulichosema." Je, hiyo ni kweli? "Kitakuwa chako. Si Mimi; kitakuwa *chako*." Ni nguvu za aina gani zimepewa Kanisa!

Kwamba, sasa, unaweza kulitamka kwa dhana za kiakili . . .

180 Lakini kama ikifanyika ufunuo halisi wa Mungu, ambapo unaliona kabla halijatukia, na kulitamka katika mfano wa neno, neno hilo linashikilia na kufanyika mwili; wazo lililotamkwa! Loo, jamani, jinsi Mungu angeweza . . . Mnaliona? Moyo wako na akili yako ziko hivyo, na zimejazwa na Roho wa Mungu, mpaka mawazo yako yanakuwa mawazo Yake. Amina. Haya basi. Wakati nia yako, na uongozi wako, na uelekezi wako, vinakuwa mahali pa moja kwa moja, au uvuvio wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu ambao unatenda kazi na mwili wako wa kibinadamu! Loo, jamani!

181 Tunapaswa kuwa watu wa aina gani? Ikiwa Roho Mtakatifu mwenyewe amekuingia sana, au kukutia nguvu, hata hutumii mawazo yako mwenyewe, hutumii akili yako mwenyewe, hutumii maoni yako mwenyewe; lakini Roho Mtakatifu amekujenga sana, mpaka mawazo yako na utu wako ni Roho wa Mungu akijieleza Mwenyewe kupitia kwako! Tungekuwa kanisa la aina gani?

182 Ingekuwa ni watu wa namna gani, asubuhi ya leo, kama Maskani hii ya Branham, asubuhi ya leo, ingejazwa sana na Uwepo wa Mungu, mbona, wakati hata hukutumia akili yako mwenyewe, hata hutumii mawazo yako mwenyewe, hata huna mwisho wako mwenyewe, ila kuongozwa tu na Roho?

183 "Na wale walio wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu." Ndipo wakati asili ya mwanadamu inapotoka, naye Roho wa Mungu anaijaza nafasi hiyo, ambapo umejiweka tupu, amina, wakati huo ndipo Kanisa, katika Nguvu Zake za kufufuka kwake Bwana Yesu, litakwenda katika hatua Zake, katika Nguvu Zake, katika mawazo Yake, katika Utu Wake, katika mwendo Wake! Mnaona ninachomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ndipo mawazo yako yatakuwa maneno, nayo maneno yatakuwa mwili. Hiyo ni, wakati, Kanisa katika Nguvu zake.

184 Ninaamini liko njiani, ambapo Kanisa litakuwa limevikwa Kristo sana, Roho Mtakatifu, binadamu wamejiweka mbali sana na nafsi zao, hata hawajioni, hawana [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ila kumtumikia Mungu. Nayo mawazo yao yanaendelea mbele. Wanayakataa mambo ya ulimwengu. Wanatembea tu katika Roho, wanaishi katika Roho, wanatembea katika Roho, wanaenenda katika Roho, hivyo wanatimiza sheria ya Kristo. Ndipo, upendo wa Kristo uko katika moyo wa mwanadamu, ukitembea katika Roho Mtakatifu, Kanisa hilo kuu la ajabu litasonga mbele kwa Nguvu na Uungu; kwa sababu Uungu utafunuliwa ndani ya wanadamu, na Roho Mtakatifu, akitimiza, mawazo ya nia zao.

185 Mawazo yetu yanakimbia vinginevyo. Mara nyingi tunajitokeza, tunasema, "Unaendeleaje ndugu?" Wala

hulimaanishi moyoni mwako. Mara nyingi tunasema, "Mimi ni *hivi* na *vile*. Nitafanya *hivyo*." Hulimaanishi moyoni mwako. Unaona? Silimaanishi moyoni mwangu.

186 Lakini unapoweza kufa sana kwa mambo ya ulimwengu, hata Kristo ndiye wa kwanza, Kristo ndiye yote, basi umbile lako lote ni la Roho wa Bwana Yesu Kristo. Ana udhibiti mkamilifu. Hapo ndipo mawazo yako yatakuwa safi. Mawazo yako yatatakasika. Moyo wako! Moyo wako!

Watu wengi husema, "Vema, dini inatoka moyoni mwako."

187 Hakuna uwezo wa kiakili katika kiumbe hicho kidogo kiitwacho "moyo." Huwezi kuwazia kwa moyo wako. Biblia ilisema, "Aonavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Huwezi kuwazia kwa moyo wako. Huwezi, maana hakuna kitu cha kiakili mle cha kuwazia. Yesu hakuwa anazungumza juu ya mtu wa kimwili; alikuwa akizungumza juu ya kiumbe cha kimbinguni.

188 Sisi ni viumbe vyenye sehemu tatu; nafsi, mwili, roho. Tunajua vile mwili huu ulivyo, tunatambua hilo; uko *hapa*. Tunajua roho ni nini; inautawala mwili. Lakini nafsi ni nini? Nafsi ni tabia ya roho.

189 Mtu anapoongoka, haimaanishi kwamba. . .Hili hapa fundisho zuri, lenye kilindi. Natumaini mnalipata. Wakati fulani uliopita. . .Nilikuwa tu nikiwaambia wavulana fulani hivi majuzi.

190 Mtu mmoja aliketi barazani pangu, akasema, "Ndugu Branham, wakati mmoja nilikuwa mfanyabiashara. Nami nimetumia miaka mingi, nikijaribu kuokoka." Huku akiniambia shida zake zote. Akasema mke wake alishuka akaenda na kumpokea Roho. Wala asingeweza. . . Yeye, "asingeweza kumpata Roho."

191 Nikasema, "Una maana gani, ndugu?" Naye akaniambia alikotoka, na akajielezea. Akasema. . .Nikasema, "Ati unajaribu kuokoka?"

Akasema, "Naam. Ninajaribu kuokoka."

Nami nikasema, "Bwana anataka. . . "

192 Kasema, "Ninaamini nimevuka mpaka, Ndugu Branham, ambapo huwezi kuokoka."

Nikasema, "Loo, sijui."

193 Akasema, "Angalia, nilienda kwenye mikutano ya Billy Graham, mhubiri mashuhuri, maarufu." Naye ni mtu wa ajabu wa Mungu, akimfanyia Mungu kazi kuu. Naye akasema, "Nilienda kwenye mikutano yake, naye akasema, 'Wote wanaotaka kuokoka, inueni mikono yenu.'" Kisha akasema, "Niliinua mkono wangu, kisha nikaingia kwenye chumba cha maulizo." Kasema, "Ndipo wakaniambia, kule nyuma,

ilinibidi kumkubali Yesu." Kisha kasema, "Nilipiga magoti na kuomba. Naye akaniambia, 'Sasa je, unamwamini Yesu Kristo?' Nikasema, 'Naam,' kasema, 'ninamkubali kama Mwokozi wa binafsi.' Kasema, akasema, 'Sasa umeokoka.'" Kasema, "Hakuna kitu kilichotokea kwangu."

194 Kasema, "Nikaenda basi kwa miaka kadhaa, nami nikakutana na Wamethodisti Huru, ambao walisema ilinibidi 'kufurahi vya kutosha kupaza sauti.'" Naye akasema, "Wakaniombea, na kila kitu, mpaka nikapata furaha vya kutosha kupaza sauti." Kasema, "Wakasema, 'Sasa umempata. Umepata utakaso.'" Kasema, "Nikatoka nje." Kisha kasema, "Nilikuwa nikitafuta yote niliyoweza." Kasema, "Bado sikuwa Naye."

195 Kasema, "Nikaenda kwenye mikutano ya Ndugu Roberts, Oral Roberts." Akasema, "Waliingia chumbani na kuniambia ilinipasa kumpokea Roho Mtakatifu, pia ilinibidi 'kunena kwa lugha' la sivyo sikumpata." Kasema, "Nikarudi mle ndani, nao wakaninii . . . wakaniombea, na—na kuniambia niongee na Bwana." Ki—kisha kasema, "Ni—nikanena kwa lugha."

196 Akasema, "Ndugu Branham, bado sijampata." Akasema, "Sijui la kufanya."

Nikasema, "Sasa, ndugu yangu . . . "

197 Akasema, "Nimekuwa huko Shreveport, Sauti Ya Uponyaji, nao wakaniambia ya kwamba wewe ulikuwa nabii; nije hapa na ungeweza kunifunulia, Roho akikushukia, shida yangu ilikuwa nini."

198 Nikasema, "Ndugu, si lazima uwe nabii kufanya hivyo. Neno la Mungu linatatua hilo." Nikasema, "Haihitaji unabii."

199 Nikasema, "Ndugu yangu, jambo pekee, umechanganyikiwa tu." Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani. Je, sikuzote ulimpenda Bwana Yesu?"

200 Akasema, "Naam, ni—nilikuwa mfuasi wa kanisa la Presbiteri, lakini," kasema, "Nilikwenda tu huko."

201 Nikasema, "Naam, nataka kukuuliza. Ilikuwaje, nini kilifanyika, hata ukabadilisha nia yako mara moja?"

202 Akasema, "Vema, mke wangu, yeye alishuka kwenda kwa Wapentekoste na," kasema, "akampokea Roho. Na kwa hivyo basi akarudi, na," kasema, "alikuwa na furaha." Kisha kasema . . .

Nikasema, "Ulifikiria nini kuhusu hilo? Je, ulilikosoa?"

203 Akasema, "La." Akasema, "Niliwazia tu, 'Vema, nitaona muda litakalochukua.'" Kisha kasema, "Liliendelea." Kasema, "Alionekana kuwa Naye."

204 Naye akasema, "Siku moja, nilikuwa nikiingia kutoka kufanya mauzo huko nje kwenye kitalu, ikawa nilitia mkono

mfukoni mwangu, na mtu fulani alikuwa amenipa kitini kidogo cha kale." Kisha kasema, "Nikaketi ofisini na kuanza kusoma kitini hiki." Kisha kasema, "Hisia mbaya sana ikanijia, ya kwamba yanipasa kujiweka sawa na Mungu." Akasema, "Nimekuwa nikitafuta, tangu wakati huo."

205 Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani? Wakati hisia hii ilipokujia, hujawahi kujitoa kwayo?"

Akasema, "La, bwana, sijawahi."

206 Nikasema, "Vema, hapo ndipo ulipompokea Kristo." Nikasema, "Haimaanishi 'kuinua mikono yako.' Hilo ni sawa. 'Kunena kwa lugha,' hilo ni sawa." Kisha nikasema, "'Kupaza sauti,' hilo ni sawa. Lakini hizo ni sifa za Kristo akiisha kuingia." Nikasema, "Kumpokea Kristo ni kupokea Mtu, Kristo Yesu. 'Kumpokea Yeye, ni Uzima.'" Nikasema, "Kupaza sauti, kunena kwa lugha, na madhihirisho yote," nikasema, "hizo ni sifa zinazofuata Hili. Lakini, kwanza, ni kumpokea Kristo."

207 Akasema, "Basi, Ndugu Branham, hivi nimekuwa nimeokoka wakati huu wote?"

Nikasema, "Hakika. Angalia," nikasema, "je, unampenda?"

Akasema, "Kwa moyo wangu wote."

Nikasema, "Wakati mmoja hukumpenda."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

"Na sasa unampenda?"

Akasema, "Naam, hiyo ni kweli."

"Vema, ulikuwa Naye wakati wote."

208 Ndipo akaruka kutoka barazani, akaanza kulia, na kunishika mikononi mwake. Na kusema, "Ee Mungu, nimekuwa Mkristo miaka hii yote."

209 Mnaona, jambo ni kwamba, yeye hakuwa amenyooshwa, hapo mwanzo. Haleluya!

210 Ati nini? Usingeweza kumfanya mwana-kondoo kutokana na nguruwe, hata ufanye nini. Yeye ni nguruwe, kwanza kabisa; anashika lake, na kumwambia mwana-kondoo ashike lake. Njia pekee ambayo ungeweza kumfanya nguruwe huyo kuamini ya kwamba ni vibaya kuwa katika zizi la nguruwe, ingekuwa ni kutia roho ya mwana-kondoo ndani yake. Iwapo atawahi kuwa na nafsi ya mwana-kondoo ndani yake. . . Ama, mwana-kondoo hana nafsi. Lakini laiti angalikuwa na roho ya mwana-kondoo ndani yake, asili yenyewe ya kitu hicho! Hiyo ndiyo sababu huwezi kumfanya, kumgeuza nguruwe, huwezi kumgeuza mwana-kondoo, kwa sababu yeye hana nafsi. Kile alicho, katika roho yake, ana asili iyo hiyo milele. Unaona?

211 Lakini, mwanadamu anaweza kubadilishwa kutoka nguruwe akawa mwana-kondoo, kwa sababu ana nafsi iliyoumbwa kwa mfano wa Mungu. Amina.

212 Naam, mawazo yake yalibadilika. Kitu fulani kinamfanyia hivyo. Haleluya! "Aonavyo mtu moyoni mwake." Mnaona? Kristo Muumba akamjia, katika umbo tulivu, na kuumba. Roho Wake Mwenyewe aliiondoa asili ya mtu huyo, ya kupenda kucheza dansi, na ulimwengu, na kufanya yasiyofaa, na tangu wakati huo aliiweka tu kando na akawa na njaa kwa ajili ya Mungu. Naye Mungu alikuwa ndani yake wakati wote. Ilikuwa ni Mungu, hapo mwanzo. Mnaona? Haya basi. Amina.

213 "Aonavyo mtu." Inabidi iwe ni wazo kabla haijaweza kuwa neno. Nalo neno, likitamkwa, hudhihirika. Ninaamini moyoni mwangu kwamba mimi ni Mkristo kwa sababu nimemkubali Bwana Yesu Kristo; nisipolia, nisiposogea, nisipofanya jambo lolote. Moyoni mwangu, kwanza, ninaamini kwamba Kristo alinifia badala yangu. Amina. Ninalikubali, kama Mkristo; ninaliamini, kama Mkristo; basi liko moyoni mwangu. Ndipo ninalitamka kama neno, "Mimi ni Mkristo." Haleluya! Ndipo ninaanza kutembea kama Mkristo, kuzungumza kama Mkristo, kuishi kama Mkristo, kuwa kama Mkristo. Na kwa matunda yangu ninatambulikana, na ulimwengu, kama Mkristo. Haleluya!

214 Aisee, sikukusudia kupaza sauti hivyo. Lakini, lakini Hilo hapo, Neno la Mungu! Yesu alisema . . . Hili hapa! Loo, niambieni tu wakati nimetumia muda sana. Lakini, vema, Yesu alisema hivi. Angalieni, "Hapo mwanzo." Angalieni. Mnaona, "Mtu, aonavyo moyoni mwake." Sasa sikilizeni kile Yesu alisema. Hatutapata . . .

215 Loo, laiti ungalisafiri kote na kuona hizo dini; na moja haina budi kufanya *hivi*, na moja haina budi kufanya *vile*, na moja haina budi kufanya *vile*. Lakini, ndugu, hebu na tuache maskani hii ya kale, wakati mmoja, hebu tunyooshwe milele.

216 Sisi ni Wakristo, kwa imani. Kwa neema ya Mungu, sisi ni Wakristo. Mnaona? Mungu, katika rehema Zake zisizo na kikomo, alituita tupate kupatanishwa Naye, kwa njia ya Mwanawe, Kristo Yesu. Inalitatua! Sio yale tuliyofanya. Yale aliyofanya Yeye; aliibadilisha nafsi yangu kutoka kwa mambo ya ulimwengu, kuelekea mambo ya Mungu; kutoka katika mbio za farasi, na kucheza kamari, na uzinzi, na kusema uongo, na kuiba. Alibadilisha nafsi yangu, akabadilisha mawazo yangu; ndipo mawazo yangu yakawa halisi sana mpaka yakawa maneno midomoni mwangu; nayo yakafanyika mwili, na sasa mimi ni Mkristo. Ilinifanya mtu tofauti. Hicho ndicho kilichokufanya. Unaona?

217 Sasa, kama una nia mbili, wala huamini Hilo, "Naam," unasema, "vema, nashangaa tu." Afadhali uwe mwangalifu!

218 Unasema, "Vema, ndugu, ni—nilikuwa na wakati mzuri." Sijali ulikuwa na wakati mzuri kiasi gani. Useme, "Naam, nimepaza sauti." Hilo ni jema, lakini hilo bado halilimaanishi.

Wasema, "Nimenena kwa lugha." Hilo ni jema, lakini hilo—hilo bado halilimaanishi. Unasema, "Nimewaponya wagonjwa." Hilo bado halilimaanishi.

219 Yesu alisema, "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, waseme, 'Je, sijatoa pepo kwa Jina Lako, nikafanya mambo makuu?' Atasema, 'Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata siwajui.'" Naam, bwana.

220 Paulo alisema, "Nijaposema kwa lugha, na wanadamu na Malaika, nijapokuwa na imani ya kuhamisha milima, nijapotoa mali zangu zote kuwalisha maskini, kama sina upendo, si kitu mimi."

221 Inapaswa kuwa ni mabadiliko. Hili hapa, badiliko la moyo; si la kitu hiki cha kimwili, bali moyo wa nafsi yako. Kitu fulani ndani, kinatia nanga, mpaka mawazo yako upande huo ni butu; huoni hayo tena. Unamwona tu Bwana Yesu. Unaona haki, na utakatifu, na usafi, na upendo, na neema. Hapo ndipo umebadilishwa. Mwongofu ni nini? *Kuongoa* maana yake ni "kubadilisha kitu." Nayo mawazo yako, tabia zako, utu wako, umebadilishwa kutoka mwenye dhambi ukawa Mkristo. Jambo la kwanza, unajua hilo moyoni mwako; kisha unalitamka kwa midomo yako; ndipo linafanyika mwili, na hivyo ndivyo ulivyo.

222 Sasa, ikiwa unafikiri kwamba unalifikiria, (neno la jinsi gani!), lakini unafikiri unaliwazia, nawe unalitamka wala halifanyiki mwili, basi umepitia njia mbaya. Mnalipata? Labda afadhali nininii. . .niongee polepole kidogo. Angalia, iwapo unadhania wewe ni Mkristo, nawe ulitamke kwa midomo yako, lakini ukagundua kwamba sivyo ulivyo, afadhali ubadilishiwe mawazo yako, badilisha moyo wako. Unaona? Kwa sababu, haushuhudii, hauzai matunda yake. "Lakini tunda la Roho ni upole, amani, uvumilivu, wema, rehema, imani." Iwapo kila kitu kidogo kijacho, nawe unakirukia, afadhali uwe mwangalifu. Kuna kitu fulani hakijafanyika. Unatamka kitu fulani *hapa*, ambacho hakipo *hapa*.

223 Yesu aliwaambia Mafarisayo, "Enyi wanafiki! Mnawezaje kusema mambo mazuri?" Hilo ndilo lililowafanya mnafiki; waliwazia jambo moja moyoni mwao, huku wanatamka kwa midomo yao jambo lingine. Huyo ndiye mnafiki. Hilo ndilo linalomfanya mtu mnafiki. Kasema, "Mwawezaje, mkiwa mnafiki. Maana, kinywa cha mtu hunena yajazayo moyo wake. Hamneni yale mnayowazia hasa." Basi mnaona ninachomaanisha? Inakubidi kusema unachowazia. Ikiwa huliwazii, usiliseme. Unaona? Nena maneno yako, acha yatoke ndani kabisa ya moyo wako.

224 Kama Yesu alivyosema juu ya mti ule, "Mtu asile kwako." Mbona, hakukuwako—hakukuwako na kivuli cha shaka moyoni mwake mwote, kwamba mti huo ungenyauka. Kwa nini? Moyo Wake ulikuwa ukitoka kwenye ninii safi, kutoka. . .Ilikuwa ni

Roho wa Mungu ndani Yake, ambaye alikuwa akimfanya hivyo, akiwafundisha wanafunzi hao somo. Mnaona ninachomaanisha? Vema.

225 Basi, acha huo uwe safi. Acha mawazo yako yawe safi, na matamshi yako yawe safi. Ishi safi na uwe safi. Sasa, kutoka moyoni mwako hutoka "mawazo mabaya, uzinzi," na mambo haya yote mbalimbali; kama hayo yakitoka moyoni mwako, hayo ndiyo yaliyo moyoni mwako. Lakini endapo kutoka moyoni mwako huja "haki, amani, upendo, furaha," loo, jamani, basi inatoka kwenye rasilimali *hapa* ambayo imefanyizwa kwa hayo. Mnaona ninachomaanisha? Imefanyizwa kwa Roho wa Mungu *hapa* ambaye anajidhihirisha Mwenyewe kwa matendo, na yale usemayo basi yatatimia.

226 Nitawapa ufahamu kidogo wa jambo fulani, jinsi Neno la Mungu lisivyoweza kukosea. Angalia usemacho. Mungu anaponena jambo lolote, halina budi kutimia, sijali jinsi linavyoonekana tofauti. Nimeona mambo, kama vile katika ratiba hii yenyewe sasa hivi. Nimemwona Mungu akifanya jambo fulani, enyi marafiki, ambalo nilifikiri kamwe haliwezi kutendeka, bali lilitendeka. Baada ya kuona kosa la kitu fulani nilichofanya, lilikuwa ni kosa; nilipaswa kufanya jambo fulani. Mungu aliniambia, nenda ukalifanye; nililiandika hapa mfukoni mwangu. Na badala ya kufanya hivyo, nilisahau, ndipo nikageuka na kufanya jambo lingine. Ndipo neema ya Mungu ikalizungusha moja kwa moja na kulimaliza, kwa vyovyote vile. Amina. Halina budi kutukia.

227 Vema, ninaamini, hapa katika Yohana Mtakatifu, nilikuwa tu nikipasoma hivi majuzi, mahali fulani hapa, jambo lile lile. Yapata, hebu tuone, huo ni wa 12. Naam, hili hapa. Angalieni, Yohana Mtakatifu 12, na kifungu cha 37. Sikilizeni, 36, tunaanza.

> *Maadamu mnayo nuru, iaminini hiyo nuru, ili mpate kuwa wana wa* hiyo *nuru. Hayo aliyasema Yesu, akaenda zake, a—akajificha wasimwone.*

228 Sasa sikilizeni. Hili hapa. Sasa angalieni hili, kwa makini sana. Nimeliweka alama hapa. Nilikuwa nikilisoma katika . . . huko Bombay.

> *Walakini ajapokuwa a—amefanya miujiza mingi namna hiyo mbele zao,* mnaona, *hawakumwamini:*

229 Haidhuru alikuwa amefanya nini! Alifanya miujiza. Angalieni taifa hili, angalieni watu hawa, angalieni ni ishara gani na maajabu yametukia papa hapa katika maskani hii. Angalieni mambo ambayo yamesemwa, na yale ambayo yamethibitishwa kuwa ni ya Mungu. Angalieni! Oneni! Yamethibitishwa na Mungu, na, hata hivyo, watu humu mjini watalicheka, kulidhihaki, waseme, "Ni telepathia ya kiakili, au kitu kingine." Hawaelewi. Sikilizeni hapa.

*. . . ajapokuwa amefanya miujiza mingi namna hiyo mbele zao, hawakumwamini:*

*Ili litimie lile neno la nabii* Isaya *. . . alilosema, Bwana, ni nani aliyezisadiki habari zetu? na mkono wa Bwana umefunuliwa nani?*

*Ndiyo sababu hawakuweza kuamini, kwa sababu . . .* Isaya *alisema* hili,

230 Mungu anaposema lolote, halina budi kutukia; kwa maana ni wazo Lake kwanza, kisha Neno Lake linadhihirishwa. Basi si kitu . . . Haidhuru kijacho au kiendacho, halina budi kutimia. Loo, mnaweza kuona kutoweza kukosea kwa Neno? Loo, jamani!

*Ameyapofusha macho yao, ameifanya mizito mioyo yao; wasije wakaona kwa macho yao, wakafahamu kwa* mioyo *yao, wakaongoka, nikawaponya.*

231 Angalieni! Mungu, kupitia nabii Wake, Isaya, mtu ambaye alikuwa na mema na mabaya yake kama tulivyo nayo, alikuwa na makosa yake kama tulivyo sisi, lakini Mungu alimfanya mtu huyo ajitolee sana, kwa kuwa ni nabii, hata maneno yake: mawazo ya Mungu! Haleluya! Mawazo ya Mungu yakitamkwa kwa midomo hiyo ya kibinadamu ya Isaya; mtu mwenye dhambi na vitu nilivyo navyo mimi, akiwa na mema na mabaya yake kama nilivyo nayo, na kama ulivyo nayo; lakini chombo kilichojitolea kwa Mungu, kililitamka hilo wazo, wazo la Mungu, kwa neno. Na haijalishi walifanya nini, maneno ya Isaya yalipaswa kutimizwa, kwa maana lilikuwa ni wazo la Mungu lililodhihirishwa kupitia Isaya.

232 Haya basi. Haleluya! Ee Mungu! "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda." Loo, jamani! Wakati ulimwengu haupo tena, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Kwa nini? Alikuwa akitamka, katika Neno, wazo la Mwenyezi Mungu. Basi wakati sisi, kwa imani, tunapoweza kulikubali Neno hilo, halina budi kufanyika mwili. Loo, jinsi linavyoufurahisha moyo wangu, kuwazia, "Neno Lako, milele, Mbinguni, Bwana, limethibitika." Mawazo ya Mungu yapo, Yeye huyatamka katika Maneno, na hili *Hapa* Neno lililo hai la Mungu.

233 Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Haleluya!

234 Si "yeye aendaye kanisani." Si "yeye awekaye jina lake kwenye kitabu." Si "yeye anayekiri." Si yeye "apazaye sauti." Si "yeye awaponyaye wagonjwa." Si "yeye afumbuaye macho yaliyopofuka." Si "yeye anenaye kwa lugha." Si "yeye atoaye unabii."

235 "Bali yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali tayari amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Loo, ndugu, hebu imani hiyo itie nanga wakati mmoja katika moyo huo, mpaka Maneno hayo yawe kweli mbele za Mungu. Basi, mbingu na nchi zitatikisika na kutoweka, bali Neno hilo la Milele, wazo hilo lililoko moyoni mwako, ambalo limedhihirishwa na Mungu, haliwezi kushindwa si zaidi ya vile maneno ya Isaya yangeweza kushindwa.

236 Kumekuwako na maelfu wakitazama miujiza hiyo iliyofanyika, na hata hivyo hawangeweza kuamini, kwa sababu Isaya alikuwa amelinena na kusema, "Hawatalisadiki."

237 Neno la Mungu ni la Milele. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Mungu, hapo mwanzo, kule nyuma alipouona ulimwengu, aliniona mimi na wewe hapa asubuhi ya leo. Alimwona mtoto wangu mchanga ameketi kule nyuma. Alimwona kila mtu mwenye njaa nchini India. Alimwona kila mhubiri mimbarani. Alimwona kila mnafiki akitembea. Aliona kitu hicho chote. Nia ya Mungu isiyo na kikomo ililiona hilo.

238 Naye akasema, "Sasa, ili kukomboa jamii hiyo iliyoanguka, nitamtuma Mwanangu, Kristo Yesu." Kulikuwa na Neno. Hapo mwanzo, kabla halijakuwa Neno, lilikuwa ni wazo. Hapo awali, lilikuwa ni wazo; likatamkwa katika neno; naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu. Haleluya! Miaka milioni kumi, labda, kabla ya ulimwengu kuumbwa, Wazo la Mungu liliuona mwili Wake, amefanyiwa maskani katika mwili, ili kuondoa uchungu wa mauti. Whiu!

239 Jinsi Neno la Mungu lilivyo la Milele! Loo, nyakati zitabadilika, miaka itakuja na kupita, vipindi vya wakati vitapita; lakini Neno la Mungu litadumu milele. Hilo hapo!

240 "Ee Bwana, nijalie nilifiche Neno Lako moyoni mwangu, nisije nikakutenda dhambi. Jalia nilitafakari, mchana na usiku. Jalia niandike amri Zako juu ya besera Yangu. Na jalia daima ziwe mbe—mbele Zangu. Na, Bwana, nisije nikakutenda dhambi moyoni mwangu." Lakini jalia nitembee ndani Yake. "Kwa hiyo sasa hakuna hukumu," Warumi 8:1. Haleluya! "Hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wanaoenenda si kwa kufuata mambo ya mwili, bali kwa kufuata mambo ya Roho." Amina.

241 Mawazo ya Mungu yaliyodhihirishwa, ndani ya moyo wa mwanadamu, yanasonga mbele moja kwa moja, huku Mungu asiyepatikana na mauti akiwaongoza raia Wake mahali mahali. Nayo Biblia ilisema, "Hatua za mwenye haki huamrishwa na Bwana." Loo, jamani! Ulimwengu ni mpya kiasi gani? Umilele una urefu gani! Tunapowazia juu ya Neno la Mungu

lililotamkwa kupitia midomo ya mwanadamu, hata hivyo tunajitiisha sana kwa Neno la Mungu!

242 Alisema, "Isaya alinena habari zake. Wala wasingeweza kufanya hivyo, kwa sababu Isaya alikuwa amelisema chini ya uvuvio."

243 Yesu Kristo huyo, yule Imanueli hapa duniani, pamoja na Maandiko yote kutoka kila mahali. Wakati akitembea duniani, alijua ya kwamba angefufuka, siku ya tatu. Kwa nini? Kwa sababu Daudi, chini ya uvuvio, alisema, "Sitaiacha nafsi Yake kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Alisema, "Kwa hiyo moyo wangu ulifurahi na mwili wangu ukafanywa . . . umefurahi." Wakati Yesu, chini ya neno moja, upako, kunena . . . alinena kwa Mungu kupitia mtu aliyekuwa na mema na mabaya yake, Daudi. Daudi alisema, "Sitaiacha nafsi Yake kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu."

244 Yesu alisema, "Livunjeni hekalu hili, nami nitalisimamisha katika siku tatu." Haleluya! Aliamini Neno la Mungu lisilopatikana na mauti. Naam, bwana. Haijalishi . . .

245 "Hakusema, hakusema hivyo," unasema. "Vema, unajua, Yeye alikufa Ijumaa, na akafufuka. Vipi kuhusu 'siku tatu?"

246 Yesu alijua, katika saa sabini na mbili huja ya kufa . . . huja uharibifu mwilini. Alijua, wakati fulani kati ya siku hizo tatu, wakati fulani hapo ndani, Mungu angeufufua. Kwa sababu Daudi, chini ya uvuvio, alisema ya kwamba angeufufua. Haleluya! Andiko moja lililoandikwa katika Biblia! Alisonga mbele kama shujaa, hadi mautini, akijua ya kwamba Mungu angelitimiza Neno Lake; kile ambacho Mungu aliwazia, kwanza, halafu akakitamka. Haleluya!

247 Kwa hivyo, leo, ninaamini kwamba, "Bwana Yesu huyo aliyepaa Juu, yuaja tena, vivyo hivyo, kama mlivyomwona akienda." Naye anakuja kwa ajili ya Waliokombolewa ambao wamezaliwa mara ya pili, waliooshwa kwa Damu. "Kama alivyoenda, ndivyo atakavyokuja." Imetajwa katika Biblia. Wafalme wanaweza kuinuka, tofauti zinaweza kuja, ngurumo zinaweza kuisimamisha dunia, njaa, mabomu ya atomiki, na chochote kile. Lakini, "Yesu Mwana wa Mungu atakuja tena jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda," kwa maana ni Neno la Mungu lililovuviwa lililosema hivyo.

248 Ninaamini kweli kwamba Mungu angeuponya mwili huu, mgonjwa, kwa sababu alisema, "Alijeruhiwa kwa makosa yangu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tulipona." Acha walimu, theolojia, chochote kinachoweza kutokea, seminari ziinuke na kuanguka, lakini Neno la Mungu litasonga mbele vivyo hivyo. Naam, bwana. Mungu alisema hivyo. Na kabla Mungu hajalisema,

ilibidi liwe ni wazo. Naye Mungu aliliwazia jambo hilo lote, na kulidhihirisha katika Maneno Yake, nalo ilibidi lifanyike mwili.

249 Si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikisoma, ama niliona mahali, ambapo msichana mmoja alikuwa akiweka vizungusho hivi kwenye saa, akivichovya kwenye radiamu. Basi ilitokea aliramba hii, brashi kwa ulimi wake. Ikamwua. Miaka na miaka baadaye, walichimbua fuvu lake la kichwa; nao wakaweka darubini zao masikioni mwao, na kadhalika, na kuichomeka kwenye hilo fuvu la kichwa. Nawe ungeweza kusikia radiamu hiyo, "rru-rru-rru." Haina mwisho. Inaendelea tu mbele na mbele na mbele na mbele na mbele. Radiamu haina mwisho. Inaendelea kusonga mbele. Baada ya miaka na miaka na miaka, na fuvu halikuwa chochote ila mfupa mweupe, hiyo radiamu ilikuwa bado inapita pale kwa sababu aliitia kinywani. Sehemu yake namna hiyo, nayo radiamu inasonga mbele.

250 Ni zaidi sana vipi basi Mungu wa Milele, kupitia Utu wa Uungu Wake, na nguvu zilizonenwa za Neno Lake, anaponena Neno Lake! Nyakati zitabadilika, watu watabadilika, mataifa yatabadilika, ulimwengu utabadilika; bali Neno hilo linasonga mbele zaidi na zaidi, milele na milele, maana ni wazo la Mungu kabla ya kutamkwa. Haleluya!

251 Ninampenda kwa moyo wangu wote. Na baada ya kuona mamia ya dini za ulimwengu huu, nasema, asubuhi ya leo, "Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nitasimama; sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao, sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao."

Na tuombe!

252 Baba wa Mbinguni, loo, jinsi nilivyo na furaha asubuhi ya leo, kujua kwamba neema Yako ya ukombozi, Mwanao, ametukomboa kutoka katika maisha ya dhambi. Loo, ninapoona mwili wangu mwenyewe ukinyauka, ukizeeka, ukiingia mvi na kupata makunyanzi, hata hivyo najua ya kwamba ng'ambo ya kivuli hiki hapa, huko ng'ambo, uko mwili usiofanyizwa kwa mikono. Huko ng'ambo uko ule usiopatikana na mauti, ukingojea; na kwamba, siku moja, wakati uhai utakapotolewa kwenye mwili huu, utaamka, mpya, katika Uwepo Wake huko ng'ambo, uwe pamoja Naye katika nyakati za wakati.

253 Mungu, jalia kila mwanamume na mwanamke, asubuhi ya leo, walio na tumaini hili ndani yao, wajitakase na mambo ya ulimwengu. Na vitu hivi vidogo vya kale ambavyo vingewakokota chini, na kuwafanya wenye mashaka, jalia wawe Wakristo wenye furaha wanaokutumikia. Tujalie mambo haya, Baba, katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

254 Nafikiri nilipitisha muda kidogo tu kwenu, lakini moyo wangu ulichukuliwa na Neno Lake, juu ya Utu Wake. Nilikuja bila kujitayarisha, bila kujua nitatoa hotuba; ilitokea tu nimesema maneno haya. Na sikupata ila kifungu kimoja

kutoka katika Maandiko, lakini labda katika Jumapili chache tutalichukulia hapo na kuendelea, kile Neno lilichokuwa.

255 Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sikiliza, rafiki yangu Mkristo. Ikiwa kuna neno lolote moyoni mwako dhidi ya mtu yeyote, waendee sasa na mkapatanishwe. Myasahau yote yaliyopita. Na ikiwa umekuwa na maisha ya kupanda na kushuka, kumbuka, kitu fulani kimeingia ndani ya moyo huo, kitu kimeingia kwenye mawazo hayo. Haidhuru adui yako ni nani, mpende. Mpende. Haijalishi nini kimetokea, achana nacho. Hata hivyo, uko kwenye shamba pamoja na magugu, tunatambua hilo, lakini sote hatuna budi kukua pamoja. Hatuna budi kukua pamoja.

256 Kwa maana, kisima kizuri hakiwezi kutoa maji mabaya, wala kisima kibaya hakiwezi kutoa maji mazuri. Mti hauwezi kuzaa matunda mabaya na matunda mazuri kwa wakati mmoja. Kwa hiyo hebu ama tufanye kisima chote safi, au tukichafue kisima chote; mojawapo, mnaona. Kwa maana, kwanza kabisa ni kichafu, kwa hiyo hebu tuvisafishe visima asubuhi ya leo, na kusema, "Bwana, mimina Roho wako, na uniongoze, Ee Mungu, niongoze."

257 Kwa kuona jinsi tunavyoshuka kwenye ka—kanisa Katoliki kule, kule Rumi, nao walitaka kunipeleka kwenye kile wanachokiita kanisa la Mifupa. Na watawa wao, kwa mamia ya miaka, waliwachukua na kuwalaza chini, huko kanisani, na kuwazika. Karibu kila kanisa ni makaburini. Nao wanawaingiza jamaa hao mle ndani. Na baada ya kukaa humo muda mrefu sana, wanaenda kuwafukua. Baada ya mwili kuoza ukawa mavumbi, wanawafukua.

258 Nao wametengeneza chumba, kikubwa, kikubwa mara nyingi kuliko hiki, kwa mifupa ya binadamu tu, jinsi walivyokitengeneza na kuilundika pamoja. Na pembeni, unaposhuka chini namna *hii*, mafuvu ya vichwa na kila kitu. Taa za mwanga zimetengenezwa kwa vipande vidogo vya vidole na mifupa. Taa zimetengenezwa kwa mifupa, na kila kitu. Hakuna kitu ila tu . . . Na kuna makaburi ya wengine wanaooza. Ishara, mwishoni, ya kushangaza sana, ilisema, "Wakati mmoja tulikuwa kama ninyi, na wakati mwingine mtakuwa kama sisi." Hiyo ni kweli.

259 Na ni wale tu wanaompenda Mungu watakaopata Uzima usiopatikana na mauti. Na hiyo ni kweli.

260 Nami niliona pale, kulikuwa na watu wakija. Dini ya Kikatoliki imejaa ushirikina na kadhalika. Hayo mafuvu juu ya watawa hao pale, yalikuwa yamesuguliwa mpaka yakawa meupe. Baadhi yao yamelika, kwa kina kirefu *hivyo*; bali watu wanayasugua, wakijaribu kupata baraka na kadhalika namna hiyo, kutoka kwenye mafuvu ya watawa hawa. Inaonyesha tu, ni mwanadamu. Ni moyo, nao wana njaa ya kitu fulani.

261 Ndugu, dini ya Yesu Kristo haijumuishi kusugua mifupa ya wafu. Inamwamini Bwana Yesu Kristo, na kuukubali Uzima usiopatikana na mauti. Loo, jamani!

262 Lakini kuwazia kwamba ni kweli, wakati mmoja watu hao walikuwa kama sisi tulivyo hapa asubuhi ya leo. Walikuwa na nafasi yao, nasi tuna yetu. Utafanya nini nayo?

263 Loo, fanya kila wakia wake uhesabiwe kwa Bwana Yesu. Usiwe na wakati kwa mambo ya ulimwengu. "Weka kando kila mzigo mzito ukuzingao kwa upesi. Hebu tupige mbio kwenye mashindano haya, kwa subira, ambayo yamewekwa mbele zetu." Tumpende Bwana Yesu.

264 Iweni na fadhili ninyi kwa ninyi. Iweni na fadhili kwa adui zenu. Mpende kila mtu. Haidhuru walifanya nini, wapendeni, hata hivyo. Na kama huwezi kufanya hivyo, ndugu, dada, kama basi kuliwahi kuwa na wakati ulipohitaji . . .?. . . madhabahuni, ni wakati huo. Unapoweza kurudi, umba . . .

265 Basi nilitambua, hivi majuzi, roho ya ubinafsi ikija ndani yangu, ya kusema, "Mtu *huyu* amekosea. Ninapaswa kumwambia kuhusu hilo." Hilo ni kosa. Mungu Ndiye wa kumwambia hilo. Hiyo si . . . Siyo kazi yangu. Lakini kazi yangu ni kuihubiri Injili na kumpenda kila mtu, na kusonga mbele na kuwapenda adui zangu, kama Yesu Kristo alivyonipenda nilipokuwa adui Wake. Hiyo ni kweli. Nilipokuwa asiyependeka, Yeye—Yeye alinipenda mpaka kifuani Mwake. Na mtu yeyote asiyependeka, jalia niwapende vivyo hivyo. Hebu Roho aliyekuwa ndani ya Kristo, na awe ndani yetu. Amina. Nampenda. Nampenda. Loo, jamani!

> Usitamani utajiri wa ulimwengu huu usio na maana,
> Ambao huoza upesi sana,
> Tafuta kupata hizo hazina za Mbinguni,
> Hazitapita kamwe!
>
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
>
> Wakati safari yangu imekamilika,
> Ikiwa kwa Mungu nimekuwa mkweli,
> Nyumba yangu nzuri na angavu Utukufuni,
> Nafsi yangu iliyonyakuliwa itaiangalia!
>
> Basi tushikilie mkono wa Mungu usiobadilika!
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

266 Je, hayo ndiyo maombi ya kila mwanamume kwa mwanamke, mvulana au msichana, hapa ndani leo? [Kusanyiko

linasema, “Amina.”—Mh.] Mungu awabariki, na awalinde hivyo; mnyenyekevu rohoni mwako; laini nafsini mwako; ukiwasamehe wengine kama Kristo, kwa ajili ya Mungu, alivyokusamehe wewe. Kuwa mwenye fadhili, mkarimu, mkaribishi.

267 Je, kuna shughuli nyingine, chochote kanisani, Ndugu Neville?

268 Sikiliza, rafiki yangu mpendwa Mkristo, unaposafiri kutoka hapa, asubuhi ya leo. Hatuna mengi hapa ya kukupa, kwa njia ya nyenzo, ninyi wageni malangoni petu. Tuna maskani ndogo, ya kale. Sisi ni watu masikini, maskini tu kadiri tuwezavyo kuwa. Tu—tunasikitika kwamba hatuwezi kuwa na kitu bora zaidi hapa kuwakilisha ma—makaribisho kwa watu. Lakini, ndugu yangu, dada, ndani ya kuta hizi ndogo hapa, kwamba hili jengo halivutii sana, lakini utapata makaribisho ya Bwana Yesu Kristo. Njoo, abudu pamoja nasi, ikiwa huna mahali pa kwenda. Tunaye mchungaji mzuri sana hapa. Baadhi ya watu wazuri hapa kwenye halmashauri za mashemasi, na kadhalika, Wakristo wengine wazuri. Njoo, tafuta kiti, nawe daima utakaribishwa hapa kwenye Maskani ya Branham.

269 Tuna jambo moja tu tunaloweza kufanya, tunampenda Bwana Yesu kwa moyo wetu wote. Tunaamini Neno kuwa . . . Biblia hii kuwa ni Neno la Mungu. Hatuna vitabu vyovyote vya kiada; Biblia hii tu. Hatuna sheria hapa ya *hili*, *lile*, ya . . . Vema, sheria yetu ni upendo. Kanuni yetu ya imani ni Kristo. Nasi tunakupenda tu kwa mioyo yetu yote. Rudi na uwe pamoja nasi, ukipenda. Nasi tunatumaini siku moja kukuona katika Nchi bora zaidi, ambapo tutaninii . . .

270 Lakini kwa wakati huu, hebu tupige hatua kuelekea Sayuni, tafadhalini, huku mkisimama kwa miguu yenu. Teddy, naomba uje hapa, kwa dakika moja tu, mwanangu, upesi sana. Sisi ni . . .

271 Ibada ya Ushirika usiku wa leo. Loo, nina furaha kuwa hapa kwa sababu hiyo. Sikilizeni, Yesu alisema, “Aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu, yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku za mwisho.” Neno hilo halipatikani na mauti. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Vema.

272 Sasa, sote pamoja sasa, hebu na tuimbe *Twenenda Sayuni*. Vema.

> Njoni, sisi tumpendao Bwana,
> Na hebu raha yetu ijulikane,
> Jiungeni na wimbo wa maelewano mazuri,
> Jiungeni na wimbo wa maelewano mazuri,
> Na hivyo mkizunguke Kiti cha Enzi,
> Na hivyo mkizunguke Kiti cha Enzi.

Sasa geukeni na kupeana mikono.

> Twenenda Sayuni,
> Sayuni nzuri, nzuri;

Twenenda juu Sayuni,
Mji mzuri wa Mungu.

Loo, twenenda Sayuni,
Sayuni nzuri, nzuri;
Twenenda juu Sayuni,
Ni Mji mzuri wa Mungu.

273 Sasa, tunapoimba pambio hilo mara nyingine tena, kisha wimbo wetu wa kufumukana. Tutaimba *Twenenda Sayuni*, mara nyingine tena, jitambulishe kwa mgeni. Mwambie umefurahi kuwa yuko hapa. Maana, kanisa lina joto, nasi hatutakaa muda mrefu kanisani, tunaondoka. Ibada imekwisha sasa. Tutafumukana tu katika dakika chache. Sasa hebu tugeuke na kusema, "Mimi ni Bw. Jones, nami nina furaha kukutana nawe. Rudi maskanini." Iweni wa kirafiki, mtabasamu, kila mtu. Vema, sasa.

Twenenda . . .

Jitambulishe kwa mgeni, mwambie arudi.

. . . Sayuni nzuri;
Twenenda juu Sayuni,
Ni Mji mzuri wa Mungu.

274 Sasa wimbo usiopatikana na mauti wa Maskani ya Branham, tukifumukana. Ni wangapi wanaokumbuka wimbo wa zamani wa kufumukana?

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Peleka, kila uendako.

Loo, jamani! Kila mtu, pamoja.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Peleka kila uendako.

Loo Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Peleka Jina la Yesu,
Kama Ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yanapokuzunguka,
Loo, pumua hilo Jina Takatifu katika maombi.

Loo Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, (Loo, Jina la thamani!) Loo, jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

275 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa katika maombi. Mchungaji, njoo uturuhusu kutoka, tafadhali, ndugu yangu.

54-1003M Neno Lilifanyika Mwili
(Taarifa Ya Ziara Ya India)
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org